**NEEMA** yanukia Tanzania kuuza sukari ughaibuni



UKURASA 3

**MAHOJIANO MAALUM:** Mkurugenzi CMA afichua siri kuhusu uteuzi wake



UKURASA 5

**NCHEMBA** aomba Sweden kutoa zaidi misaada miradi uchumi



UKURASA 8

SUPA JACKPOT
TZS. 1,157,290,273
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Nipashe
Ijumaa Septemba 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581448
www.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

# BAKWATA: Ukabila na udini katu visitugawe

UKURASA 2



Yasisitiza kutunza amani ya nchi kwa manufaa ya wote. Yakemea ukanda na itikadi za kisiasa zinazoenezwa na watu au vikundi vyenye nia mbaya ya kutaka kuivuruga...

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Baraza la Maulid Kitaifa Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, jijini Dodoma jana. **Picha zaidi Uk. 18. PICHA: OWM**

**RIPOTI MAALUM:**

## Wataalamu waonya popo hatarini kutoweka



UKURASA 4

## Meneja TARURA adaiwa kuwatisha maofisa TAKUKURU kwa bastola

UKURASA 2



Chifu Hangaya pangapangua iendelee

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 29, 2023 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

NGO yabuni mbinu ya waliotoka magerezani kuingia katika miradi ya kujimudu kiuchumi

ULIVYO UCHUMI NA RUZUKU NCHINI

Rais Dk. Samia akanyaga mkoani Lindi na ufafanuzi neema anayowaachia shambani

• Waziri Bashe afafanua ruzuku inavyopandikizwa, kumvusha mkulima

Na Mwandishi Wetu

Rais akizungumza wiki iliyopita, alipokuwa ziarani mkoa wa Lindi. PICHA: MTANDAO.

UKURASA 11

MICHEZO YANGA : TUTATINGA MAKUNDI CAF HIVI UK. 24

KATUNI UK. 6

HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande (kulia), akiwasili kwa ajili ya kuzindua Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) 2023), jijini Arusha jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU iliyoandaa mkutano huo, Ludovick Utouh. Habari Uk. 3. **PICHA: SANULA ATHANAS**

# BAKWATA: Ukabila, udini katu visitugawe

**Na Romana Mallya**

BARAZA Kuu la Waislamu wa Tanzania (BAKWATA), limewataka Watanzania kutokubali kugawanywa kwa misingi ya udini, ukabila, ukanda wala itikadi za kisiasa.

Katika salamu zake za Baraza la Maulid Taifa zilizofanyika jijini Dodoma jana na kusomwa na Katibu Mkuu BAKWATA, Alhaji Nuhu Mruma, alisema ni muhimu kutunza amani ya nchi kwa manufaa ya wote.

"Tusikubali kuigawa nchi yetu kwa misingi ya udini, ukabila, ukanda au itikadi za kisiasa zinazoenezwa na watu au vikundi vyenye nia mbaya ya kutaka kuvuruga amani yetu. Hili halikubaliki.

"Tunawaomba sana wanasiasa na wadau wengine tutumie fursa hii kujijenga na kujiimarisha kisiasa na tusitumie majukwaa ya siasa kueneza chuki na matusi dhidi ya wengine," alisema.

"Tunaipongeza serikali na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kuisimamia na kuitunza amani ya nchi yetu kwa kushirikiana na wananchi," alisema.

Aidha, alisema BAKWATA imebaini takwimu zinaonyesha idadi ya watu wanaojitokeza kupiga kura imekuwa ikishuka na kuwafanya viongozi waliochaguliwa wawe wamepigiwa kura na kundi dogo la wale wanaowaongoza.

Kutokana na hali hiyo, BAKWATA imeiomba serikali wakati wa kuelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu ujao, taasisi za dini zishirikishwe huku wakitaka kuimarishwa zaidi mfumo wa elimu ya uraia na elimu ya mpigakura.

"Iimarishe kwa kuzishirikisha taasisi zetu za dini na kujenga ubia katika utekelezaji wa jambo hili, kwani bado wananchi wengi wana imani kubwa sana na mhimili huu wa taasisi za dini.

"Wakati tukielekea katika chaguzi hizo, takwimu zinaonyesha idadi ya watu wanaojitokeza kupiga kura imeshuka na kuwafanya viongozi waliochaguliwa wawe wamepigiwa kura na kundi dogo la wale wanaowaongoza," alisema.

Mruma alisema bila shaka zipo sababu za kushuka kwa namba ya wanaojitokeza kupiga kura, ikiwamo kukosa elimu sahihi ya mpiga kura, umuhimu wa uchaguzi, michakato isiyo sahihi ya kupata wagombea kutoka katika vyama vya siasa, rushwa kutawala kipindi cha uchaguzi.

Alisema mambo haya yote yanasababisha kukosekana kwa haki katika uchaguzi, kunakosababishwa na watu wachache wasio na uzalendo.

Kadhalika, alisema BAKWATA wana uhakika wa ushirikishwaji mkubwa wa taasisi za dini utasaidia kuongeza hamasa ya wapiga kura na wengi watajitokeza kupiga kura katika chaguzi mbalimbali.

Alisema katika kuadhimisha Maulid ya mwaka huu iliyobebwa na kaulimbiu; "Maulid, Maadili na Maendeleo" upo umuhimu mkubwa wa waislamu kujua maisha ya Mtume Mohamed katika kuelewa na kuufuata Uislamu.

Pia, BAKWATA imeomba serikali itoe msamaha wa ada ya maji ya visima kwa misikiti yote yenye huduma hiyo kutokana na mamlaka ya Bonde la Wami, Ruvu au Mto Pangani kuvitoza baadhi yake.

Alisema jukwaa kama hilo ni sehemu mojawapo ya mawanda ya kujifunza na kuelewa maisha ya Mtume Mohamed, ambaye ni zawadi na rehema kwa walimwengu wote, katika misingi ya maadili ya kuigwa na watu wengine.

"Tunaposherekea leo hii, tunaona suala la mporokomo wa maadili katika nchi yetu ni suala mtambuka na kama kuna lawama zozote katika hili, wa kwanza kulaumiwa ni familia.

"Tunapaswa kujitathmini viwango vya maadili katika familia, ni kweli kwamba tupo chini ya uadilifu tunapaswa kuchukua hatua na kurudi katika uadilifu," alisema.

Alisema BAKWATA inatoa wito kwa jamii kusimamia malezi ya watoto, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watoto wanafundishwa elimu ya dini tangu utotoni na kuzoea ibada.

Katika maadhimisho hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa ufafanuzi kuhusu ombi la ushiriki wa madhehebu ya dini katika kutoa elimu ya uraia kwa wapiga kura, alisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ina utaratibu maalum wa kuendesha mchakato huo na wakati ukifika tangazo litatolewa ili taasisi zenye sifa ziweze kuomba na kupata kibali hicho.

"Ninawasihi sana viongozi wa madhehebu ya dini endeleeni kushirikiana na serikali kwa kuwahamasisha waumini kuwa na utulivu pamoja na kujitokeza kwa wingi katika michakato yote inayoendelea kabla ya uchaguzi ikiwamo kushiriki katika maboresho ya daftari la mpiga kura," aliomba.

Alisisitiza kuwa, serikali inawategemea na kwamba, kauli yao ina nguvu na inakubalika na kuwataka waendelee kuwahamasisha wananchi kushiriki katika hatua zote kuelekea uchaguzi kwa amani.

Kuhusu ombi la msamaha wa ada ya maji ya visima, Majaliwa alizielekeza mamlaka za mabonde zikutane na viongozi wa dini na kusikiliza changamoto zao na kupeleka mapendekezo ya namna bora ya utekelezaji kwa kuwa suala hilo liko kisheria.

"Toeni mapendekezo yenu na serikali iko tayari kuyapokea na kuyafanyia kazi. Serikali ni ya maridhiano, nami naamini kupitia kikao hicho muafaka utapatikana kwa pande zote," alisema.

# Sera, usimamizi wa fedha yaleta matokeo chanya

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, amesema kuwapo kwa sera nzuri, usimamizi wa fedha na uwezeshaji katika kilimo kumeleta matokeo chanya kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa zinazozalishwa na wakulima wadogo na wa kati.

Alisema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akifunga warsha ya siku moja iliyokuwa ikijadili namna bora ya kuwekeza katika sekta ya kilimo kwa maendeleo endelevu ya taifa.

Warsha hiyo iliandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya kuwainua wakulima wadogo kiuchumi (MEDA) iliyokuwa na lengo la kuwakutanisha pamoja wadau wa kilimo nchini.

Dk. Hashil alisema warsha hiyo ni matokeo ya mkutano wa kimataifa wa masuala ya kilimo uliofanyika Dar es Salaam hivi karibuni chini ya usimamizi na uongozi imara wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Naipongeza taasisi isiyo ya kiserikali ya kuwainua wakulima wadogo kiuchumi kwa kuwakutanisha pamoja wadau wa kilimo nchini katika warsha hii iliyokuwa na majadiliano ya namna bora ya kuwekeza katika sekta ya kilimo kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu," alisema.

Mwakilishi Mkaazi wa Taasisi hiyo, Mussa Lubango, alisema lengo kuu la kuwapo kwa warsha hiyo ni kuwainua wakulima wadogo na wa kati katika sekta ya uchumi na maendeleo endelevu.

Vile vile, kuwapo muunganiko kama huo utatoa fursa ya masoko kwa wawekezaji katika kuzalisha mazao mbalimbali ya kibiashara na chakula nchini.

"Pongezi kwa serikali kupitia kwa wizara husika kwa kutupa ushirikiano mzuri na kuwezesha warsha hii kufanyika nchini kwani tunaiona Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula katika ukanda wa Afrika na Mashariki ya

# Meneja TARURA matatani madai kuwatisha TAKUKURU kwa silaha

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

MENEJA wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Misungwi, Mhandisi Bright Mndeme, ameingia matatani kwa madai ya kutishia kuwapiga risasi viongozi akiwamo ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Kutokana na madai hayo, Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Paul Chacha, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa wilaya (OCD), Mrakibu Mwandamizi (SSP) Oskar Mmole, kumnyanganya silaha hiyo.

Mndeme anadaiwa kuwatishia maofisa hao kwa silaha walipomfuata kwa ajili ya kumchunguza kuhusu tuhuma za kupokea rushwa kutoka kwa mkandarasi ambaye ameshindwa kutekeleza mradi wa barabara kwa wakati.

Chacha alitoa agizo hilo juzi alipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Nyanshishi - Fela yenye urefu wa kilomita nane ambayo ilitakiwa kukamilika Septemba Mosi, mwaka huu, lakini mpaka sasa haijakamilika na mkandarasi hajatoa taarifa yoyote.

Mkuu huyo wa wilaya alisema meneja huyo alipofuatwa na maofisa wa TAKUKURU kuchunguza madai ya kupokea rushwa ya Sh. milioni 15, alitishia kuwapiga risasi.

"Na wewe meneja wakati wanakutafuta unaanza kusafisha bastola yako na kusema kuwa atakayekusogelea aidha umuue au ujiue mwenyewe. Nakuagiza OCD mnyang'anye hiyo silaha afuate utaratibu upya wa kumiliki silaha," aliagiza Chacha.

Aidha, Chacha alimwagiza Mkuu wa TAKUKURU Wilaya kuendelea na uchunguzi juu ya vitendo vya rushwa vinavyoelezwa kufanywa baina ya watumishi wa TARURA na mkandarasi mwenye zabuni ya kutekeleza mradi huo wa ujenzi wa barabara hiyo na miradi mingine.

"Baada ya kuona Kamanda wa TAKUKURU anafuatilia sana kuhusu hii Barabara, maofisa wa TARURA walifungwa midomo kwa kutumia Sh. milioni 15 ili taarifa zisitolewe na mkandarasi akitafutwa juu ya utekelezaji wa barabara hii anadai kuwa yuko busy (ana kazi nyingi). Huyu hatufai," alisisitiza Chacha.

Mkuu huyo wa wilaya pia alimwagiza katibu tawala wa wilaya kumchunguza mkandarasi aliyepewa zabuni ya barabara hiyo inayogharimu Sh. milioni 212 ambayo serikali imeshalipa Sh. milioni 100.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo waliomba serikali kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo pamoja na kuchimba mitaro ambayo inadaiwa kumwaga maji katika makazi yao kutokana na kutokutengenezwa vizuri.

"Hapa mvua zikinyesha maji yanaelekea kwenye makazi pamoja na kusomba udongo wa barabara na kuharibu miundombinu na makazi yetu. Tunaomba wajitahidi kutengeneza mitaro na kutuondolea adha tunayokumbana nayo," alisema Amos Taikadansu, mkazi wa Nyangomango.

HABARI KITAIFA

# Habari njema Tanzania kuuza sukari ughaibuni

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema kutokana na jitihada za uzalishaji wa sukari zinazofanywa na viwanda vya ndani, kuna uwezekano mkubwa Tanzania kuanza kuuza bidhaa hiyo nje ya nchi ndani ya miaka miwili ijayo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah, alisema hayo jana wakati yeye na makatibu wakuu wenzake watatu walipotembelea kiwanda cha sukari cha Kagera kuangalia uzalishaji.

Makatibu wakuu waliotembelea kiwanda hicho, mbali na Dk. Abdallah, ni wa Wizara ya Fedha Dk. Natu Mwamba na Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli.

Dk. Abdallah alisema walitumwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, kwa ajili ya kuangalia uzalishaji wa sukari kiwandani hapo.

Alisema wameridhishwa na teknolojia inayotumika kiwandani hapo kuzalisha bidhaa hiyo na kwamba itasaidia kuzalisha kiwango kikubwa cha sukari itakayoondoa upungufu kwa matumizi ya ndani.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameweka sera na mazingira wezeshi kwenye sekta ya viwanda na Juni, 2022 alikuja hapa kiwandani kuweka jiwe la msingi la awamu ya tatu ya upanuzi wa kiwanda. Kwa hiyo sisi wasaidizi wake lazima tuje tuangalie maendeleo ya kiwanda," alisema.

Pia alisema ziara ya makatibu wakuu hao ni moja ya mkakati wa serikali kuhakikisha inajitosheleza kwa chakula na bidhaa zingine kama sukari ili kuachana na utamaduni wa kuagiza bidhaa nje ya nchi.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji kujenga viwanda vya sukari ili kuhakikisha inajitosheleza kwa sukari na miaka michache ijayo iachane na tabia ya kuagiza nje. Dk. Abdallah alisema Mwenyekiti wa Chama cha Wazalishaji Sukari Tanzania ambaye ni mmiliki wa Kiwanda cha Kagera, Self Ally Seif, amewahakikishia kwamba uzalishaji wa sukari unaendelea vizuri kwenye viwanda mbalimbali hapa nchini.

"Na uzuri ni kwamba mmiliki wa kiwanda hiki Seif ndiye mwenyekiti wa umoja wa wazalishaji sukari Tanzania kwa hiyo ametupa takwimu zinazoonyesha kwamba ndani ya miaka miwili tutakuwa na uwezo wa kujitosheleza wenyewe kwa sukari na kuuza nje ya nchi.

"Ile ndoto ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Tanzania kuilisha Afrika na dunia kwa ujumla sasa inaanza kutafsirika kwa vitendo na suala la kuagiza sukari nje ya nchi sasa linaenda kufikia kikomo tutailisha Afrika na dunia kupitia kiwanda cha Kagera Sugar," alisema.

Alisema upanuzi wa kiwanda cha Kagera unakwenda vizuri kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu ambayo imesababisha uzalishaji kutia matumaini kwa kuwa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka na kwa mwaka huu pekee, wameahidi kuzalisha tani 15,000.

Alisema kiwanda hicho kinapanga kuzalisha tani 300,000 kwa mwaka kitakapokamilisha upanuzi wa awamu ya nne na hivyo kuifanya Tanzania kutokuagiza sukari nje ya nchi, kuongeza kiwango cha ajira na kulipatia taifa fedha za kigeni.

Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Tobi Nguvila, alisema uongozi wa mkoa huo utamlinda mwekezaji huyo kwa kuhakikisha hapati changamoto zozote kwa kuwa ameajiri wananchi 115,000 kutoka mkoani humo na amekuwa akichangia shughuli mbalimbali za kijamii.

Naye Self alisema anaunga mkono juhudi za serikali za kutaka kuilisha dunia kwa kuanza na uzalishaji wa sukari na mnyororo wa thamani unaotoa ajira nyingi na kuongeza pato la taifa kupitia fedha za kigeni.

# Mpango ataka wananchi washirikishwe mikakati kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema kuna haja serikali za Afrika kuongeza uwazi na kushirikisha wananchi katika mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jana kupitia hotuba yake iliyosomwa na Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande, wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) 2023, unaofanyika jijini Arusha. Makamu wa Rais alisema mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari kubwa kwa jamii, hivyo ni muhimu kuwapo uwazi katika matumizi ya fedha zinazotolewa na wadau kuyakabili, pia ushirikishwaji wa wananchi. Alipongeza Taasisi ya WAJIBU kwa kuratibu mkutano huo unaofanyika kila mwaka tangu mwaka 2021, ukiwa na lengo la kuhimiza uwazi na uwajibikaji kwa serikali na taasisi. Alisema fedha nyingi zimekuwa zinatolewa na wadau mbalimbali katika kuendesha miradi ya kijamii, hivyo suala la uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha hizo haliepukiki. Alikumbusha kuwa wakuu wa nchi na serikali za Afrika walipokutana kwa siku tatu jijini Nairobi, Kenya mwanzoni mwa mwezi huu (Septemba 4-6) kujadiliana kuhusu mabadiliko ya tabianchi, walitoka na azimio la kuyaona mabadiliko ya tabianchi kama kikwazo kikuu kwa ustawi wa watu na tishio kwa usalama wa dunia.

Alisema nchi nyingi za Afrika sasa zinakabiliwa na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi, yakijumuisha mvua isiyotabirika, mafuriko na mlipuko wa moto katika misitu, yote yakisababisha madhara kiuchumi, afya, elimu, amani na usalama.

"Katika dunia hii tunamoishi, migogoro mingi inasababishwa na usimamizi usio mzuri wa rasilimali za umma, mara nyingi ikitokana na uongozi dhaifu. Migogoro hiyo inatokana na matumizi ya rasilimali za umma, lakini sasa mabadiliko ya tabianchi yametikisa kiuchumi, kijamii, amani na usalama.

Alisema Tanzania inashirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza mikakati ya kubaliana na mabadiliko ya tabianchi, akisisitiza umuhimu wa uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha zote zinazotolewa kwa ajili ya mikakati hiyo.

"Licha ya Afrika kukadiriwa kuwa na asilimia 40 ya nishati mbadala, ni Dola za Marekani milioni 60 tu sawa na asilimia mbili ya Dola trilioni tatu zilizowekezwa Afrika katika mulongo uliopita kupata nishati hiyo," alisema.

Katika hotuba yake hiyo, Dk. Mpango alipongeza Taasisi ya WAJIBU kwa kuandaa mkutano huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, akiutaja ni jukwaa muhimu kujadiliana ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika kudai uwazi na uwajibikaji kiutendaji.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya WAJIBU, Yona Killagane, alisema kuna haja kuwa na uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha zinazotolewa kwa serikali na sekta binafsi kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIBU, Ludovick Utouh, alishukuru mabalozi wa nchi za Norway, Uswisi na Sweden kwa kufadhili mkutano huo.

**UCHAGUZI NA TABIANCHI**

Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, alishauri ajenda ya mabadiliko ya tabianchi iwe sehemu ya vigezo vya kupata viongozi wakati wa uchaguzi. Wanaowania udiwani, ubunge na urais wapimwe kwa mikakati yao ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi itolewe kwa wananchi ili washiriki kukabili mabadiliko ya tabianchi. Sekta binafsi nayo ishirikishwe kukabili baa hili," alishauri.

Balozi Chassot alisema kuwa kwa kuzingatia madhara makubwa yanayoshuhudiwa duniani, kuna haja ajenda ya mabadiliko ya tabianchi iwekewe mkazo kwa kuwa somo linalofundishwa kuanzia shule za msingi hadi vyuoni.

"Uandaaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 uzingatie pia suala la mabadiliko ya tabianchi ili kuwalinda wananchi dhidi ya madhara," alishauri Balozi Chassot.

Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Ozaki Macias, alishauri kuwe na uwazi serikalini katika kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi na kufadhili miradi ya kukabili madhara hayo.

"Tuweke mikakati thabiti ya kupata ufadhili kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Tuwekeze kwa ajili ya kesho na si kuila kesho yetu," alishauri.


TEMBO NICKEL

**NOTISI YA KUWAOMBA WANANCHI AMBAO WANAMILIKI ARDHI KATIKA ENEO LA MRADI WA KABANGA NICKEL WA KAMPUNI YA TEMBO NICKEL NA HAWAJAFANYIWA UTHAMINI KUWASILIANA NA KAMPUNI**

**Tarehe ya Notisi: 29, SEPTEMBA 2023**

Ardhi inatwaliwa kwa ajili ya mradi wa Kabanga Nickel (Mradi) wa Kampuni ya Tembo Nickel (Tembo Nickel) katika Vijiji vya Bugarama, Rwinyana, Muganza, Nyabihanga na Mukubu katika Kata za: Bugarama, Muganza na Bukiriro, Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera.

Imetangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 18 Agosti 2023, kwamba mwananchi yeyote ambaye anamiliki ardhi katika eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli za Mradi na bado hajafanyiwa uthamini anaombwa kuwasiliana na kampuni ya Tembo Nickel ili aweze kukaguliwa mali yake/zake kwa kufanyiwa uthamini na kulipwa fidia ya mali husika.

Kampuni ya Tembo Nickel inawaomba wananchi wote kuwasiliana na kampuni haraka iwezekanavyo ndani ya siku thelathini (30) tangu kutolewa kwa tangazo hili.

Wananchi ambao maeneo yao hayajafanyiwa uthamini wanaweza kuwasiliana na Kampuni ya Tembo Nickel kwa:

- Kupiga namba ya ya Tembo Nickel **0800 750 258** bila makato.
- Kutuma ujumbe kupitia barua pepe ya: **info@tembonickel.com**
- Kufika katika ofisi za Tembo Nickel za Mahusiano ya Jamii, Rulenge (ofisi ipo Jengo la Parokia ya Rulenge).
- Kuwasiliana na mwenyekiti wa kijiji husika:

1. Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Bugarama – Bw. Florian Mwana. Namba ya simu 0768 262 680.
2. Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Rwinyana – Bw. Evarister Kaziro. Namba ya simu 0682 106 385.
3. Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Muganza – Bw. Jackson Gwabujala. Namba ya simu 0657 928 494.
4. Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Nyabihanga – Bw. Eraldius Batakanwa. Namba ya simu 0626 876 078.
5. Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Mukubu – Bw. Hezekia Matabisi. Namba ya simu 0764 647 448.

**Kwa ajili na kwa niaba ya KAMPUNI YA TEMBO NICKEL: MRADI WA KABANGA NICKEL**
**tembonickel.com**

RIPOTI MAALUM



# Wataalam waonya popo hatarini kutoweka

Na Christina Mwakangale

WAKATI Bunge likifikishiwa kilio cha kukithiri kwa popo, maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, wataalamu wa mimea, viumbehai na wanyamapori, wamesema kuna haja ya kumlinda mnyama huyo ambaye ni kati ya walio hatarini kutoweka duniani pia ni miongoni mwa wanaotegemewa kuendeleza ikolojia.

Miongoni mwa njia zinazoshauriwa kuwadhibiti ni pamoja na kuwahasi popo wa kike, ili kupunguza kiwango cha kuzaliana eneo husika na sio kuwaondoa kwenye makazi yao ya asili, bila kufanyika taratibu za kitaalamu za kudhibiti viumbehai, ikiwamo utafiti.

Mwanasayansi wa maabara kutoka Idara ya Zoolojia na Uhifadhi wa Viumbepori Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Yusuph Wilangali, anasema iwapo popo wataongezeka, zitumike mbinu kuwaondoa ikiwamo kuwahamisha bila kuathiri ikolojia yao.

Ofisa Mtafiti Mkuu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dk. Emmanuel Mmassy, anaelezea sifa za popo na tabia yake ya kuishi mazingira tulivu na yenye giza hasa katika miti ama mapango na kurundikana kwa makundi inaweza kuwa sababu mojawapo ya mnyama huyo kutajwa na baadhi ya watu kuwa kero, ingawa ni miongoni mwa wanyama kama wengine.

Wataalamu hao walizungumza na Nipashe hivi karibuni kwa nyakati tofauti, baada ya baadhi ya wabunge kuitaka serikali, kuwaondoa popo maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ikiwamo wakazi wa jiji hilo kuzungumzia kero inayosababishwa na mnyama huyo kwenye makazi yao.

Bungeni Septemba 4, mwaka huu, wakiuliza maswali, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mgaya alihoji ni lini serikali itaondoa popo maeneo ya Upanga, huku swali la nyongeza, likitoka kwa Mbunge wa Viti maalum (CCM), Mariam Kisangi, likihoji kuhusu suala hilo.

Mariam alisema kumekuwapo tatizo la popo maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam na kuongezeka siku hadi siku hali inayosababisha uharibifu wa kuvunja vioo vya madirisha kwenye baadhi ya nyumba.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alisema wizara imeendelea kudhibiti popo katika jiji hilo, kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubaini ukubwa wa tatizo na mbinu rafiki kimazingira zitakazotumika kuwadhibiti.

Baadhi ya wakazi wa Upanga, jijini Dar es Salaam, waliozungumza na Nipashe, walieleza kero wanazokumbana nazo, huku Flodge Mtepa, mlinzi wa Shule ya Msingi St Columbas, ambayo imezungukwa na miti iliyojaa popo, alisema anatumia muda wa ziada kuwakabili.

"Hawa popo nawakimbiza kuanzia saa 10 au 11 alfajiri, napanda juu ya mti na kipande cha bati na fimbo ya kupiga bati, ukiwapigia kelele ndio wanatoka. Saa 11 jioni pia napanda tena nawapigia kelele wanatoka, hivi hivi hawawezi kutoka," anasema Mtepa.

Amesema hutenga muda wa saa moja kila siku kuwafukuza ili kuleta utulivu na muda ambao kunakuwapo ahueni ni usiku majira ambayo wanyama hao huenda kutafuta mlo mbali na makazi yao.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Pili Kikola, anasema kwa muda mrefu wanyama hao wamekuwa kero, hasa ikizingatiwa eneo hilo ni la shule.

"Popo ni changamoto sana, popo tunaambiwa walikuwapo wenye historia wanasema ni muda mrefu wapo hapa, nasi tumewakuta ingawa wanasema kipindi hiki wamezidi. Wanaleta usumbufu mkubwa na alfajiri tunalazimika kuwatuma walinzi wapige mabati, hawapendi kelele," anasema.

"Sisi tunawafukuza na wakienda eneo lingine wanafukuzwa, wanarandaranda wanarudi tena hapa hapa. Mvua ikinyesha eneo linanuka harufu yao, miti yote sasa imekuwa na vipara wanaharibu, miembe, miashoki, minazi, kwa ujumla ni waharibifu na miti wanachagua ya kukaa yenye utomvu hawakai, kama michikichi, mwarobaini."

Aliziomba mamlaka husika kutafuta mbinu za kuwaondoa kwa kupunguza matawi ya miti au kuikata, akisema jitihada zingine walizozifanya zimegonga mwamba na walipojaribu kukata miti, walitakiwa kuomba kibali.

"Popo wanakaa hasa kwenye miti ya asili na huu uliopo hapa ni mti wa siku nyingi, ila umeshaelemewa na popo ni wengi mno. Tulitaka kuukata mti walikojaa tukaambiwa hadi kibali, hatujapewa kibali hadi sasa. Wamekuwa kero wanachafua kuta za nyumba na wamehamia hata katika miti tuliyoipanda kwa ajili ya kutunza mazingira, baada ya mti wa asili kuelemewa."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Sea View, Victor Muneni, anasema tatizo la popo limeongezeka eneo lake, huku TAWIRI, ikiwa ni miongoni waliopiga hodi mtaa wake mara kadhaa, kwa ajili ya kufanya utafiti.

"Popo wapo eneo lote, Upanga Mashariki na Magharibi, wanakaa katika miti yote isipokuwa yenye utomvu. Tumejaribu kupunguza miti na maeneo ilikopunguzwa matawi wamepungua, kwa sababu wanapenda kukaa kwenye miti mirefu," alisema Muneni.

**MTAALAMU UDSM**

Mwanasayansi wa Maabara kutoka Idara ya Zoolojia na Uhifadhi wa Viumbepori Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wilangali, akizungumza na Nipashe kwa undani kuhusu mnyama huyo, anasema popo ni aina ya wanyama mamalia ambao wamo kundi moja na wanyama wenye nywele, chuchu na wanaonyonyesha watoto wao waliowazaa.

"Popo ni kama binadamu, simba na swala, tofauti na uvumi. Popo wapo wa aina nyingi takribani 1,400 duniani ambayo ni asilimia 20 ya 'species' walio kwenye kundi la mamalia. Iwapo tunataka kuwahamisha kama wakazi wanavyosema ni kero, nashauri kwanza utafiti ufanyike kabla ya kuwahamisha.

"Zipo njia nyingi, lakini lazima izingatiwe ikolojia na eneo wanalohamishiwa, ikimbukwe popo anaweza kuruka hadi kilomita 59 kwenda kutafuta chakula na kurudi tena kwenye makazi yao. Njia hii ya kuwahamisha pia ni nzuri, kwa sababu hatuwaui au kuwangamiza," anasema mtaalamu huyo.

Anasema popo wanategemewa kwenye mfumo wa kiikolojia na kutegemewa na mimea kadhaa kwa kufanya uchavushaji, hivyo iwapo wataondolewa kwa kuwadhuru, mimea pia itaathirika.

"Kwa Dar es Salaam hasa eneo la Upanga wapo popo ambao kitaalamu tunawaita 'fly fox' kwa sababu sura yao ni kama mbwa ila wanaruka. Nashauri ufanyike utafiti labda zitengenezwe kemikali ambazo zikiwekwa mahala walipozidi watahama eneo hilo, ila tujihakikishie usalama wa viumbe wengine," alisema Wilangali.

Aidha, mtaalamu huyo anaonya aina nyingine ya kuawaondoa kama vile kukata miti au matawi, kuwavuna kama mlo kwa kuwa baadhi ya jamii nchini ambazo huwatumia popo kama kitoweo, inaweza kuwaondoa duniani wanayama hao moja kwa moja na kuathiri mazingira,

"Katika maeneo mengi ya Afrika, tayari imeonekana aina hii ya popo wanapungua kwa kasi, kwa sababu wanaliwa na wamewekwa kwenye hatari ya kutoweka duniani kutokana na kupungua. Sishauri kufanyika mbinu ya kuawaua, kwa sababu kimaadili kwa wanyama hii haishauriwi," alisema Wilangali akiongeza;

"Nilipopita Upanga nilibaini wanakaa katika miti ya kupandwa ambayo ni kwa ajili ya kivuli huwa inasambaa kwa juu, miashoki, miembe na mingine. Maeneo mengi hasa Afrika popo wameonekana kuwa kero, ila tatizo linaweza kushughulikiwa ma mamlaka husika, hawa ni nyara za serikali kama wanyapori wengine."

MAHOJIANO MAALUM

# Mkurugenzi CMA afichua siri uteuzi wake

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni, aliyekuwa Ofisa Mfawidhi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mpulla, aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Tume hiyo. Katika mahojiano aliyofanya na mwandishi wetu, Mpullu anaeleza mambo aliyopitia katika kazi ya usuluhishi hadi kuteuliwa kwake...

**SWALI: Kwanza, hongera kwa kuaminiwa na kuteuliwa katika nafasi hii.**

**JIBU**: Asante. Kwa kweli namshukuru Mungu. Natambua haikuwa rahisi.

**SWALI: Inawezekana watu wengi wamesikia jina lako baada ya kutangazwa kuwa Mkurugenzi wa CMA. Nini safari yako katika masuala ya uamuzi na usuluhishi?**

**JIBU:** Mimi si mgeni CMA. Niliajiriwa CMA Juni 21, 2010 nikiwa mwamuzi daraja la pili na kituo changu cha kwanza kilikuwa Tanga. Nilifanya kazi hadi mwaka 2016 katika nafasi hiyo. Aliyekuwa ofisa mfawidhi, Haji Kayugwa, alihamishwa ndipo nikateuliwa kuwa Kaimu Ofisa Mfawidhi Kanda ya Tanga.

Wakati huo Tanga ilikuwa na ofisi Muheza, Lushoto na Korogwe. Ilipewa hadhi hiyo kwa sababu kulikuwa na migogoro mingi ya kazi. Tulifanya kazi za usuluhishi ikiwamo kuelimisha umma ili kumaliza migogoro haraka hali ambayo ilisababisha takwimu za usuluhishi wa migogoro ya kazi kupanda sana.

Jambo la kwanza jamii inapaswa kujua kwamba jukumu kubwa la Sheria ya Kazi (Sheria ya Kazi na Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004) ni kuchochea ukuaji wa uchumi. Waajiri na wafanyakazi wanapaswa kuzalisha ili kukuza uchumi badala ya kuwa katika migogoro. Tuliona ili kutimiza azma hiyo, tuliweka kipaumbele katika kutatua migogoro ya kazi ili kukuza uchumi kwani kuwapo kwa migogoro kunakwamisha uzalishaji.

Zamani kesi zinazohusu migogoro ya kazi zilikuwa zinafunguliwa katika mahakama za kawaida. Hali hiyo ilisababisha mrundikano wa kesi hatua ambayo ilisababisha watu kutumia muda mwingi mahakamani huku uzalishaji ukisimama na hatimaye uchumi kudorora. Kutokana na hali hiyo, serikali iliamua kuanzisha Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kuharakisha utatuzi wa migogoro ya kazi.

Kama nilivyosema awali, usuluhishi wa migogoro ya kazi Tanga ulipanda sana. Kipekee, niwashukuru waliokuwa wakuu wa mkoa, Meja Jenerali (mstaafu) Said Kalembo na Martine Shigella. Walitoa ushirikiamno mkubwa kutimiza azma hii ikiwamo kutumia redio za ndani kutoa elimu. Vyama vya wafanyakazi mkoani Tanga vilitoa ushirikiano mkubwa sana.

**SWALI: Nini kilitokea baada ya mafanikio hayo?**

**JIBU**: Baada ya kufanikisha kwa kiasi kikubwa utatuzi wa migogoro Tanga, mwaka 2017 nilithibitishwa kuwa Ofisa Mfawidhi wa Kanda ya Tanga.

Nirudi nyuma kidogo, nakumbuka nikiwa Tanga, mwaka 2017 kulikuwa na maadhimisho ya sherehe za Mwenge na kaulimbiu ilihusu kuchochea ukuaji wa uchumi. Katika maadhimisho hayo, kulikuwa na kongamano na nilimwomba Mkuu wa Mkoa (wakati huo Shigella) niwasilishe mada, aliniruhusu. Mada yangu ilikuwa 'Uhusiano wa Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi na Ukuaji wa Uchumi'.

Katika kongamano lile alikuwapo aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya kazi, Anthony Mavunde (sasa Waziri wa Madini). Wengi waliifurahia na wakafahamu uhusiano wa utatuzi wa migogoro na ukuaji wa uchumi.



Usekelege Mpulla

**SWALI: Baada ya hapo nini kilitokea?**

**JIBU:** Mwaka 2018 nilipata uhamisho kwenda Kilimanjaro kuwa Ofisa Mfawidhi. Wiki mbili baada ya kuripoti, lilitolewa agizo la serikali kuhamia Dodoma, hivyo CMA pia ilitakiwa kutekeleza agizo hilo.

Baada ya kuhamia Dodoma, menejimenti ya CMA ilitafakari nani aende Dar es Salaam. Wakati huo Dar es Salaam ilikuwa na asilimia 40 ya mashauri yanayohusu migogoro ya kazi Tanzania nzima.

Nikiwa Kilimanjaro, nilipewa taarifa kuwa natakiwa kuhamia Dar es Salaam kuwa mfawidhi wa kanda. Nilishtuka kwa sababu wakati huo nilikuwa bado. Nilijiuliza ni kitu gani kimesababisha nihamishiwe Dar es Salaam. Pia ilijiuliza, sawa nimeongoza Tanga ikiwa na ofisi nne lakini Dar es Salaam ina watu wengi, nitawezaje kumudu?

Nilitii na Januari 9, 2019 niliripoti. Kwa jumla nilikuwa natambua changamoto zilizokuwapo kwa sababu niliwahi kuletwa katika mpango wa kuondoa mrundikano wa migogoro ya kazi. Wakati huo wastani wa mashauri 1,200 katika ofisi za CMA Temeke, Ilala, Ubungo, Kibaha hadi Mkuranga yalikuwa yanafunguliwa kila mwaka na wakati huo kulikuwa na takribani watumishi 50, hivyo ilikuwa kazi kubwa.

**SWALI: Uliweka mkakati gani kukabiliana na hilo?**

**JIBU:** Mkakati wa kwanza ulikuwa kuongeza kasi katika utatuzi wa migogoro. Lakini kubwa zaidi, staili yangu katika kufikia malengo ni shirikishi kwa kushirikiana na taasisi kama ofisi ya mkuu wa mkoa, wakuu wa wilaya na makatibu tawala wa wilaya. Watu wengi walikuwa wanakimbilia katika ofisi hizo. Kwa hiyo niliamua kuwafuata wananchi kwenye mamlaka hizo na nikasisitiza kuwa wakifika wawalete kwangu.

Watu wengi walikuwa wanakosa haki zitokanazo na migogoro ya kazi kwa kutojua sheria. Sheria inamtaka mlalamikaji kufungua shauri ndani ya siku 30 baada ya kuachishwa kazi lakini badala ya kufanya hivyo, walikuwa wanakilimbilia kwa wanasiasa.

Mkakati mwingine nilioweka ni kushirikiana na vyombo vya habari. Nilipata nafasi ya kuelimisha jamii njia bora ya kutumia huduma zetu za CMA. Nilikwenda kwenye runinga na kutoa elimu. Watu walijua umuhimu wa kutatua migogoro na hamasa iliongezeka sana. Pia nilitoa namba yangu ya simu ili mtu mwenye tatizo anipigie. Hii ilisaidia sana kuboresha huduma za CMA Kanda ya Dar es Salaam.

Jambo lingine ambalo naweza kusema lilisaidia kufanikisha azma ni kwamba aliyekuwa Mkurugenzi wa CMA, Shannes Nungu, aliniamini. Wakati huo tume haikuwa na mtu wa mawasiliano. Katika mkutano wa Baraza la Wafanyakazi, Nungu alitoa rai ya kuwa na msemaji. Kutokana na talanta yangu, ilionyesha nafaa, hivyo nilipewa nafasi hiyo.

**SWALI: Uzoefu gani mwingine ulipata Dar es Salaam?**

**JIBU:** Nikiwa Ofisa Mfawidhi Kanda ya Dar es Salaam, Tanzania iliwahi kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa SADC (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika). Katika mkutano ule niliambatana na Mkurugenzi CMA (wakati huo) na tulikutana na taasisi ya usuluhishi wa migogoro ya kazi ya Afrika Kusini (CCMA). Nilichojifunza ni kwamba sheria zetu za kazi zinaendana na za Afrika Kusini lakini wenzetu wako juu zaidi kiutendaji.

Jukwa lile lilinipa elimu na uzoefu mkubwa kuhusu usuluhishi na kumaliza migogoro ya kazi ndani ya SADC na nilipata mbinu mpya katika kuongeza thamani kwenye ufanisi ukizingatia kuwa Dar es Salaam ni eneo la kipekee. Nilijifunza kwamba huduma bora zinachangia ukuaji wa uchumi, hivyo jukumu kubwa la CMA ni kuchochea uwekezaji.

**SWALI: Awali umeeleza kuwa Dar es Salaam ilikuwa na migogoro mingi. Nini kilichangia katika kuipunguza?**

**JIBU:** Moja ya mambo tuliyofanya ni kuweka kambi za usuluhishi. Katika kipindi cha corona kwa mfano, wafanyakazi wengi waliachishwa kazi, hivyo kukawa na ongezeko kubwa la migogoro. Tilichukua waamuzi na wasuluhishi wa mikoa na kuweka kambi. Baada ya kuonyesha mafanikio, huo ukawa mpango wa taasisi.

Arusha kama inavyojulikana ni mkoa wa utalii. Sekta hii iliathirika kwa kiasi kikubwa wakati wa corona na kampuni nyingi za utalii ziliwaachisha wafanyakazi, hivyo kukawa na migogoro mingi. Ili kumaliza migogoro iliyojitokeza kwa muda, walikusanywa watumishi kutoka sehemu mbalimbali na kwenda kuweka kambi.

**SWALI: Je, hiyo ndiyo siri iliyowezesha kupunguza migogoro?**

**JIBU:** Ni zaidi ya hiyo. Nikiri wazi kuwa ushirikiano na wizara (Ofisi ya Waziri Mkuu) hasa Waziri (mwenye dhamana ya masuala ya kazi) na Katibu Mkuu ambao wametaka migogoro iishe kwa asilimia 80 pia ulichangia. Msukumo huo ulifanikisha kufikia malengo kwa kiasi kikubwa.

**ITAENDELEA KESHO**

ITAENDELEA KESHO

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kilimo hai kinaboresha afya na kuvutia utalii

**WADAU** wa kilimo wanajukumu kubwa la kuendeleza kilimo hai kutokana na faida zake kiafya na vilevile katika soko la kuvutia watalii.

Matamasha yanayohusisha bidhaa za kilimo ni lazima yatiliwe mkazo, ili yanapofanyika yasaidie kutoa elimu na kupata soko imara la mazao yanayotokana na kilimo.

Katika kutilia mkazo sekta ya kilimo, Serikali ya Zanzibar ilizindua Azimio la Utalii Endelevu lililoazimia kutangaza visiwa hivyo kuwa kivutio cha kijani na kuzitaka hoteli zote za kitalii kutumia bidhaa zinazotokana na kilimo cha visiwa hivyo.

Kilimo ni uti wa mgongo kwa sababu afya za wananchi kuwa imara inategemea kula chakula kilicho bora ambacho kinatokana na kilimo kilicho bora pia.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati akifungua tamasha la maonyesho la kilimo hai, alipongeza shughuli za uzalishaji na utengenezaji wa vitu vya asili ikiwamo ufinyanzi wa vyungu, kudarizi vikoi, ushonaji kofia za asili, matumizi ya mapakacha na masusu, mikoba ya ukili na mikeka kwa sehemu kubwa vinaendana na sera ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kusaidia kukuza uchumi.

Ukiangalia bidhaa hizo nyingi zinatokana na kilimo hivyo ni lazima kiendelezwe na kuwa bora.

Rais Mwinyi amesema serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau wa sekta hiyo, wamemaliza rasimu ya mikakati ya kilimo hai kwa Zanzibar na kueleza matumaini yake kuwa utekelezaji wake utakuwa suluhisho la changamoto za kilimo hai hasa upatikanaji wa pembejeo za kibaiolojia, elimu kwa wakulima na wafugaji na upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, Dk. Mwinyi ameeleza serikali yake inafahamu fursa zilizomo ndani ya kilimo hai na kwamba dhamira yake iwapo mkakati ulioandaliwa ukatengenezewa programu madhubuti, utekelezaji utawapa fursa vijana kuanzisha biashara za kutengeneza viuatilifu na mbolea hai kwa kusaidia upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi na kusaidia kuitangaza Zanzibar kama kivutio cha kijani.

Vile vile kuna umuhimu wa kutoa elimu kuhusu matumizi ya mbolea za kemikali kwa watumiaji na walaji na faida katika kuimarisha lishe ili kusaidia kupunguza maradhi yasiyoambukiza kama shinikizo la damu, kisukari na moyo.

Kupitia kilimo pia kuna fursa nyingi kwa wajasiriamali kujiingizia vipato na kukua kiuchumi.


Wizara ya Kilimo pia, imeeleza azma yake jinsi inavyoendeleza jitihada za serikali kushirikiana na taasisi zote za Zanzibar zinazojishughulisisha na kilimo kwa ujumla na mafanikio yaliyofikiwa.

Wizara imeeleza inavyotoa huduma kwa wakulima wanaozalisha mazao kwa kutumia mbolea za kemikali na kuwapa elimu ya namna bora ya kutumia pamoja na kuhamasisha jamii namna bora ya kutumia viuatilifu kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji maalumu.

Wananchi wanaeleza wanavyonufaika na fursa za kilimo hai na wanavyojikita kwenye kilimo cha mazao ya viungo na mboga kwa kutumia mbinu bora za kilimo chenye tija kwa afya.

Taasisi ya Kilimo Hai Zanzibar (ZOI), imeonyesha haja kwa wakulima na jamii kuendelea kukiimarisha kilimo hai ili kuimarisha afya za watu na udongo kwa kuepuka matumizi ya mbolea zenye kemikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge

Na Joseph Mwendapole

## TIRA inanyoosha matege yaliyokuwapo kwenye sekta ya bima ngazi ya Taifa

**SEKTA** ya bima ni muhimu kwa ustawi wa jamii popote ile duniani, ikigusa mustakabali mwema wa maisha yao, kwani majanga hayana hodi.

Ni muda mfupi nchini bima ilionekana siyo kipaumbele, pengine kutokana na vitendo vya baadhi ya watu kwenye sekta, wakichelewesha malipo baada ya ajali na mambo mengine.

Danadana za njoo kesho na keshokutwa, ziliwafanya watu kukosa imani na bima. Ndiyo maana hata ukuaji wake ukawa wa kusuasua kwa miaka mingi.

Lakini, tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), hali ni tofauti, imani imeongezeka na idadi ya watumiaji bima inaongezeka maradufu.

Miaka michache tu tangu kuanzishwa TIRA, sekta imekuwa haraka kufikia asilimia 12 kutoka asilimia tano, iliyokuwapo muda fupi uliopita.

Ni jambo la kujivunia, ikionyesha dalili njema kwa Watanzania kuwa na imani na kampuni za bima, waliyoidhamini wa wapata fidia stahiki.

Ni mageuzi makubwa yaliyofanywa na TIRA ndani ya muda mfupi, kunyooshwa kwa mapito ya bima, kiasi cha wananchi sasa wanakiri kufanya vizuri, ubabaishaji ukibaki hadithi.

Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware hivi karibuni akaeleza kuwa sekta hiyo tangu kuanzishwa kwake, kampuni za bima hazina tena makando kando ya miaka ya nyuma, mtu anapopata majanga, anapata fidia inayostahili na kwa wakati.

Yale mambo ya nenda rudi ya miaka ile hayapo tena, hali inayowavutia wananchi wengi kuona umuhimu wa kukata bima, kwani sasa wana uhakika wa kupata fidia mapema. TIRA sasa inawaondoa Watanzania kwenye fikra za zamani, ikiwahakikisha kupatikana fidia mapema na kwa kiwango wanachostahili.

Kamishna anaahidi mamlaka inaendelea kuzisimamia kampuni za bima kulipa madai na fidia stahiki, tena kwa wakati na haki. Hadi sasa ulipaji madai na fidia stahiki kwa wateja wa bima yamefikia asilimia 95, hivyo kupunguza malalamiko yao.

Kamishna anataja asilimia tano ya madai na fidia, yana changamoto ambazo TIRA inafuatilia na kutoa suluhisho. Anatoa mfano kuwa ulipaji wa madai ya bima za kawaida uliongezeka kwa asilimia 10.1 kutoka shilingi bilioni 301.9 mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 332.09 mwaka 2022.

Pia anasema malipo ya madai na mafao ya bima za maisha yaliongezeka kwa asilimia 29.3 kutoka bilioni 95.7 mwaka 2021 hadi bilioni 123.71 mwaka 2022.

Vilevile, kiasi cha madai kilicholipwa mwaka 2022 ni shilingi bilioni 455.80, hivyo, imepunguza umaskini kwa wanufaika na kufanya biashara kuwa endelevu.

Anataja mamlaka imeendelea na mikutano, ikipokea na kusikiliza malalamiko ya bima kwa wananchi na baadaye, ilifanikiwa kuandaa mikutano mitano katika kanda zote za mamlaka.

Kamishna Saqware anasema Sekta ya Bima imekua kwa wastani wa asilimia 12.8% kwa mwaka ambapo kwa kipindi cha miaka mitano mauzo ghafi ya bima yameongezeka kutoka Sh.bilioni 691.9 mwaka 2018 hadi kufikia takribani Sh. trilioni 1.2 mwaka 2022.

Anasema mchango wa Sekta ya Bima kwenye pato la Taifa unazidi kuongezeka kutoka asilimia 0.56% kwa mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 1.68% kwa mwaka 2021.

Anasema mamlaka imeendelea kuongeza gawio serikalini ambapo kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 imeweza kulipa gawio kwa Serikali la jumla ya Sh. bilioni 2.9.

Kamishna Saqware anasema sekta ya bima imechangia kwenye ajira kwa vijana, hadi Septemba mwaka jana 2022 imetoa ajira za kudumu kwa Watanzania 4,173.

Anasema katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, imefanikiwa kuanzisha Konsotia ya Bima ya Kilimo, ili kutekeleza Skimu ya Bima ya Kilimo kwa ufanisi, tarehe 01 Julai 2023, kukazinduliwa Konsotia ya Bima ya Kilimo.

Pia, kiongozi huyo ana ufafanuzi kwamba, uzinduzi huo ulifanyika mkoani Tabora Waziri Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe katika kilele cha Siku ya Ushirika Duniani (SUD).

Lingine linalotajwa, kuanzishwa Konsotia ya Bima ya Kilimo, ili kuweka ufanisi katika utekelezaji Skimu ya Taifa ya Bima ya Kilimo (TAIS) na kuongeza uwezo wa kimtaji wa soko la bima nchini kwa ajili ya kukinga majanga shambani.

Anasema mtaji wa kukinga majanga yenye thamani ya shilingi bilioni 300 umetengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo.

# Waliopisha mradi wa umeme kulipwa fidia

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

WANANCHI 496 waliopisha mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Uhuru kilichoko katika kijiji cha Vumilia, Urambo mkoani Tabora, wataanza kulipwa fidia.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, huku akibainisha kuwa fedha hizo za fidia zitaanza kulipwa kuanzia mwanzoni mwa Oktoba, mwaka huu na taratibu zote za ulipaji fidia hiyo zimekamilika.

"Wananchi nawaomba muandae nyaraka zote muhimu zikiwamo barua na vitambulisho vinavyothibitisha kulipwa fidia ili Oktoba 2, mwaka huu, mtakapoanza kulipwa fedha zenu kusitokee changamoto ya aina yoyote itakayochelewesha malipo hayo. Fedha ziko tayari na taratibu zote zimekamilika," alisema Kapinga.

Pia alisema ujenzi wa mradi huo umefikia zaidi ya asilimia 66 na utekelezaji wake unaendelea vizuri.

Kapinga alisema kukamilika kwa mradi huo kutaimarisha huduma ya upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi na mingine iliyo jirani.

Mradi huo pia unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Kigoma pamoja na vituo viwili vya kupoza na kusambaza umeme vya Urambo na Nguruka.

Aidha, mradi una njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Katavi pamoja na ujenzi wa vituo vitatu vya kupoza na kusambaza umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Kapinga amewasha umeme katika kijiji cha Mtakuja wilayani Urambo huku akiwasihi wananchi kulinda na kutunza miundombinu ya umeme kwa kuwa serikali imetoa fedha nyingi kutekeleza mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Kenan Kihongosi, aliishukuru Serikali kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha upatikaji wa huduma za kijamii ikiwamo umeme, vituo vya afya, maji, shule na barabara katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Ziara hiyo ilihudhuriwa na Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta, viongozi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Kapinga alifanya ziara ya siku tatu ya kukagua maendeleo ya mradi wa usambazaji umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili katika wilaya za Nzega, Uyui na Urambo kwa kuwasha umeme katika baadhi vijiji na kuzungumza na wananchi.



Mtaalam Msaidizi wa maabara kutoka Chuo cha Afya VECTA, wilayani Muheza mkoani Tanga, Rukia Ahmed akitoa elimu kwa viongozi wa Halmashauri na wananchi kuhusu teknolojia mpya ya mashine za kuangamiza wadudu aina ya mbu majumbani na mitaani wakati wa maadhimisho ya Siku ya Afya ya Mazingira Duniani katika soko la Michungwani mapema wiki hii. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Erasto Mhina na (wa pili kushoto) ni Ofisa Afya wa wilaya hiyo, Khadija Fadhili. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Tahadhari yachukuliwa kukabili El Nino

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, imeanza kuchukua hatua za kuzuia madhara yanayoweza kutokana na mvua za El Nino kwa kuifikia mikoa iliyotajwa kuwa na dalili za kukumbwa na janga hilo.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitabiri kuwapo mwelekeo wa mvua za msimu wa vuli kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba, mwaka huu, ambao umeonyesha uwapo wa El- Nino. Katika kukabiliana na hali hiyo, serikali imeagiza mikoa na wilaya kupitia kamati za maafa katika ngazi zote, kuainisha na kuandaa rasilimali za kuzuia, kukabiliana na maafa hayo.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Anderson Mutatebwa, alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akifungua kikao kazi cha kuimarisha uwezo wa kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na madhara ya El Nino kwa kamati ya usimamizi wa maafa mkoa wa Pwani. Alisema Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Namba 6 ya mwaka 2022 na kanuni zake imeanzisha kamati za usimamizi wa maafa kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata na vijiji kuzuia na kupunguza madhara ya majanga ya aina zote na kujiandaa kurejesha hali kwa ubora zaidi endapo maafa yatatokea.

"Mikoa 14 nchini itafikiwa kwa ajili ya kupata elimu ya namna ya kukabiliana na mvua za El Nino kama vile Pwani (vikiwamo visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Kagera, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Geita, Simiyu, Morogoro na Kigoma hadi kufikia Septemba 30 (kesho)," alisema.

Katibu Tawala mkoa wa Pwani, Rashid Mchata, alisema tayari mkoa una kamati za maafa hadi kwenye vijiji na kwamba wamejiandaa vyema kukabiliana na majanga ikiwamo mvua za El Nino. Alisema suala la kukabiliana na majanga kwao ni endelevu na kwamba watahakikisha kamati za maafa zina uwezo wa kifedha ili kutekeleza majukumu yao kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kuwa salama.

Mchata alisema uwezekano wa kutokea kwa mvua za El Nino katika mkoa huo upo kutokana na historia katika miaka ya nyuma lakini pia mkoa kuzungukwa na mito na bahari, hivyo wamejiandaa kukabiliana na majanga hayo.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Waziri awapa kazi viongozi wa dini kukemea ukatili wa kijinsia

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama, amewasisitiza viongozi wa dini kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyokwenda kinyume cha maadili na kuathiri vijana na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Mhagama alisema hayo juzi wakati wa Jubilee ya miaka 25 ya upadri kwa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, Lazarus Msimbe.

Alisema viongozi wa dini wana nguvu na nafasi kubwa ya kuzungumza na jamii katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia unaoendelea hasa kwa vijana ikiwamo ubakaji, ulawiti na ushoga.

Pia aliwataka wanawake kuona umuhimu wa kusimamia malezi bora ya watoto ili kuwaepusha na makundi yanayowasababishia vishawishi vya kungia kwenye athari za matendo ya ukatili wa kijinsia.

Waziri Mhagama alimpongeza Askofu Msimbe kwa kuwa kiongozi mwenye kumtegemea Mungu, mwenye ujasiri na upendo kwa sababu pamoja na changamoto mbalimbali alizopitia katika safari yake ya upadri, hakukata tamaa aliweza kuhakikisha anafanikisha ndoto zake.

Mhagama aliwataka waamini kuzidisha maombi mbele za Mungu bila kusahau sala kwa kuwa ni hitaji bora kwa muumini yeyote. "Hatukuomba kuishi lakini kwa mpango na upendo wake Mungu ametupa nafasi ya kuishi. Hitaji la kufanya kazi ni kubwa zaidi kuliko kile tunachopata kutokana na kazi ndiyo maana hata wastaafu wanashauriwa kuendelea kujituma kufanya kazi ili kuimarisha afya na miili yao," alisema. Mhashamu Askofu Lazarus Msimbe aliitaka jamii kuendelea kuchangia ukarabati wa Kanisa Kuu la Mtakatifu Patrice kutokana na kuwa chakavu kwa sababu lilijengwa miaka mingi iliyopita na sasa zimeshachangwa Sh. milioni 10 kwa ajili ya kazi hiyo.

Makamu wa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, Padri Salvanus Kwembe, kwa niaba ya waumini, alimpongeza Askofu Msimbe kwa kuleta maendeleo kwenye jimbo hilo licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali baada ya kuingia kwenye uaskofu.

Alisema kwa miaka miwili aliyokaa katika kiti hicho, Askofu Msimbe amesogeza huduma za kichungaji kwa waumini kwa kuzipandisha hadhi parokia teule kuwa parokia na kutangaza vigango kadhaa kuwa parokia teule kutoa parokia 60 hadi kufikia 76.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliwaomba viongozi wa madhehebu ya dini kukemea vitendo viovu ukiwemo ukatili dhidi ya watoto na vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili, zikiwemo ndoa za jinsia moja.

Jubilee hiyo ilifanyika sambamba na harambee ya ukarabati wa Kanisa Kuu la Mtakatifu Patrice. Katika hafla hiyo, Waziri Mhagama alichangia Sh. milioni tano, Malima Sh. milioni moja na wakuu wa wilaya Sh. milioni mbili huku Mbunge wa Mikumi, Denis Londo akichangia Sh. milioni mbili na wabunge wote kuahidi kuchangia Sh. milioni tano.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba (wa pili kulia), akizungumza jambo wakati yeye na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, walipotembelea Kiwanda cha Sukari cha Kagera Sugar mkoani Kagera mapema wiki hii, kuangalia shughuli za uzalishaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Nchemba ataka Sweden kuweka kipaumbele kuisaidia zaidi Tanzania

**Na Benny Mwaipaja,**
STOCKHOLM

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameuomba Mfuko wa Maendeleo wa Sweden (SwedFund) kuweka kipaumbele kuisaidia Tanzania kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji ili kukuza ajira na uchumi.

Dk. Nchemba alitoa rai hiyo juzi mjini hapa alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Miradi wa SWEDFUND, Stefan Falk.

Viongozi hao walijadili masuala mtambuka ya ushirikiano kati ya Tanzania na mfuko huo.

Alisema sekta za uzalishaji, zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi, utalii na madini, zinaajiri Watanzania wengi hususan vijana na kwamba serikali imeamua kuelekeza rasilimali kubwa kupitia bajeti na programu mbalimbali kuzikuza.

Dk. Nchemba alisema wakati SwedFund ikiandaa mkakati wake mpya wa maendeleo wa miaka mitano mapema mwakani, ni muhimu kuangalia namna itakavyochangia katika mipango hiyo ya serikali.

Alisema licha ya kuongeza ajira kwa kundi kubwa la wananchi, pia itaongeza uzalishaji wa mazao yatakayoliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Mpango huo, alisema uweke bayana namna ya kuwekeza katika kuongeza tija kwenye sekta hizo kupitia teknolojia muhimu za kuongeza thamani ya mazao na namna ya kuyafikia masoko ya uhakika.

Waziri aliishukuru serikali ya Sweden kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania kwa kuchangia maendeleo katika miaka 60 ya ushirikiano katika sekta mbalimbali, zikiwamo kilimo, afya, nishati, ujenzi wa miundombinu pamoja na kusaidia kupambana na umaskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kwa upande wake, Falk alisema uhusiano wa Tanzania na Sweden ni wa kupigiwa mfano na kwamba nchi yake iko tayari kuyafanyia kazi mapendekezo na ushauri uliotolewa na Dk. Nchemba kwa kuwa sekta hizo ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi na kupiga vita umaskini katika jamii.

Pia alishangazwa na maendeleo makubwa ya kiuchumi yanayotokea Tanzania katika kipindi kifupi kilichopita licha ya changamoto zinazoikumba dunia hivi sasa na kutaka Sweden ijifunze kutoka Tanzania namna ilivyofanikiwa kudhibiti misukosuko ya kiuchumi pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei na kupanda kwa gharama za maisha.

Dk. Nchemba ambaye amemaliza ziara yake nchini Sweden, alikutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa wizara za kimkakati , na mashirika na taasisi za fedha za Sweden. Nchemba na viongozi hao walikubaliana kuimarisha zaidi ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa faida ya pande zote mbili.

# Aua mke kisha ajinyonga, mtoto ashuhudia miili

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

MKAZI wa Kitongoji cha Muembeni Bukokwa wilayani Sengerema, Kashinje Thomas (35), anadaiwa kumnyonga mke wake Noga Lugwisha (42), hadi kufa na yeye kujinyonga kwa kutumia kamba ya katani.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi baada ya mtoto wa wanandoa hao kuamka asubuhi na kukuta baba yake akining'inia kwenye kamba huku mama yake akiwa amelala kitandani na alipomwamsha bila mafanikio, aliamua kukimbia kuita majirani.

Baadhi ya majirani na mashuhuda wa tukio hilo waliiambia Nipashe kuwa baada ya kukuta miili ya wanandoa hao walichukua jukumu la kuwaita viongozi wa eneo hilo ambao baadaye waliita jeshi la polisi na kuruhusu shughuli za mazishi kuendelea.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Bukokwa, Radslaus Majura, alikiri kutokea kwa tukio hilo ambalo taarifa zake alizipata kutoka kwa majirani wa wanandoa hao ambao wote ni wakazi wa kitongoji cha Mwembeni na kusema chanzo cha tukio hilo bado hakijafahamika.

Alisema mtoto wa marehemu hao, alipeleka taarifa kwa majirani za kuomba msaada wa kumshusha baba yake aliyekuwa juu akining'inia kwa kuwa hakuweza kumshusha na mama yake aliyekuwa akimwamsha kitandani bila kuamka.

Mwenyekiti huyo aliwataja wanandoa hao kuwa ni Noga Lugwisha (42) na Kashinje Thomas Nyengela (35), wakazi wa kitongoji cha Mwembeni Kukokwa.

Diwani wa Kata ya Kukokwa, Yusuph Busumba, amelaani tukio hilo na kuiomba jamii kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi au kujitoa uhai wanapokuwa na matatizo ya kindoa kwa kuwashirikisha ndugu wa karibu kupata ushauri.

Kiongozi wa dini wa Kanisa la Faith Mission of Tanzania, mchungaji Elia Lukona, alisema tukio hilo ni chukizo kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa anayetakiwa kutoa uhai ni Mungu pekee.





Askari polisi wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wakikagua eneo la tukio baada ya wananchi wenye hasira kumuua kwa kumchoma moto kijana Ramadhani Omari (24) mkazi wa mji wa Pongwe katika kijiji cha Tanganyika, kata ya Lusanga juzi alfajiri, baada ya kumtuhumu kushiriki kuiba ng'ombe na wenzake eneo la kambi ya Kitisa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Daraja korofi linalounganisha mikoa mitatu lakamilika

**Na Allan Isack,** KITETO

DARAJA korofi katika barabara inayounganisha wilaya za Kiteto mkoani Manyara, Mvomero na Gairo Mkoa wa Morogoro, Kongwa na Kibaigwa mkoani Dodoma limepatiwa ufumbuzi wa kudumu baada ya ujenzi kukamilika.

Daraja hilo, lililopewa jina la Mama Samia Lekaita Kiseru lililoko Kata ya Sunya wilayani Kiteto, limekamilika baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kutoa Sh.milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wake.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Chang'ombe, Olgira na Mbikasi akiwa kwenye ziara ya jimbo kwa siku tatu, Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za kujenga daraja hilo lililokuwa kikwazo kwa wananchi.

Mbunge huyo alisema kujengwa kwa daraja hilo kutarahisisha usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara kutoka eneo moja kwenda lingine.

Alisema kuwa maendeleo yanayofanywa na serikali chini ya uongozi wa Rais Samia yanaacha alama kubwa na tunu katika Wilaya ya Kiteto na nchi kwa ujumla, kwa kuwa amejipambanua kuwa kiongozi mwenye kubeba maono ya maendeleo endelevu.

Hata hivyo, Ole Lekaita, alipongeza serikali kwa kukubali na kusaini mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Kongwa (Hogoro) - Kibaya - Orkesimet - Oljoro - Arusha pamoja na Barabara ya Chemba, Kiteto, Kilindi hadi Handeni mkoani Tanga.

Aidha, aliipongeza serikali kwa kurahisisha huduma za upatikanaji wa elimu kwa kujenga shule shikizi, ambapo alisema tayari mchakato umeanza wa kusajili shule hizo katika wilaya hiyo ili ziwe shule kamili.

Alisema: "Kujengwa kwa shule shikizi kutarahisisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa shule zetu, pia itakuwa ni sehemu ya uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi na kufundishia kwa walimu".

# Wafanyabiashara watumia meza kufunga barabara

**Na Tumaini Mafie,** ARUMERU

WAFANYABIASHARA wa Soko la Tengeru lililopo Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha wamelazimika kufunga barabara iendayo Moshi-Arusha kwa kutumia meza.

Hatua hiyo imekuja baada ya kutakiwa kulipa Sh. 4,500 kwa kila meza kama mapato ya halmashauri, meza ambazo walipewa na halmashauri hiyo.

Kitendo hicho kilisababisha adha kwa watumiaji wa vyombo vya moto katika barabara hiyo, ambapo shughuli za usafiri zilisimama kwa muda hadi Mkuu wa Wilaya hiyo alipofika na kutuliza ghasia hizo.

Aidha Mkuu wa Wilaya hiyo, Emanuela Kaganda aliwataka wafanyabiashara hao kurudisha meza hizo katika maeneo yao ya biashara wakati wakiandaliwa kikao cha mazungumzo baina yao na uongozi wa halmashauri hiyo, ili kuweka jambo hilo sawa.

"Niwaombe mrudishe meza pembeni kidogo wakati huu ambao uongozi wa halmashauri unakuja kuongea na nyinyi na nimeshawaambia kuwa zoezi hili ni shirikishi, hivyo watakuja kuongea na nyinyi, wekeni vizuri hayo maoni yenu ili tuje tuzungumze," alisema Kaganda.

Alisema kuwa wanatamani kuweka utaratibu wa ukusanyaji mapato vizuri na siyo kuwakandamiza wananchi, hivyo zoezi hilo litakuwa shirikishi kwa wafanyabiashara hao.

Baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo wakizungumza na Nipashe walisema kuwa meza hizo ziliingizwa sokoni hapo na baadhi ya watu binafsi, lakini wakaambiwa kuwa ni za halmashauri jambo ambalo walisema siyo kweli.

Pamela Kweka ni mmoja wa wafanyabiashara katika soko hilo ambapo alidai kuwa wanatakiwa kulipia Sh. 4,500 kila siku huku akisema mzunguko wa biashara hauruhusu kutoa fedha hizo kwa kuwa ni mdogo na biashara zao ni ndogo.

"Tulipewa meza na watu binafsi tukiambiwa ni za halmashauri, hivyo tukaambiwa tunatakiwa kulipia Sh. 4,500 tulipokataa na kuanza kupanga vitu chini tukaletewa maaskari na kutishiwa mabomu lakini ukweli ni kwamba hatutaki na hatuwezi kufanya biashara juu ya hizi meza turudishiwe zile za 1,000 ili maisha yaendelee," alisema Kweka.

Mfanyabiashara mwingine ambaye hakutaja jina lake alidai kuwa endapo mfanyabiashara atakuwa na meza tatu anapaswa kulipa Sh. 12,000 jambo ambalo alisema hakuna ushuru unaotozwa kwa Sh. 4,000 kwa meza au kizimba Arusha nzima, kwamba wanashangazwa na utaratibu huo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jeremia Kishili alipoulizwa kwa njia ya simu endapo Baraza la Halmashauri la Wilaya ya Arumeru lilishawahi kupitisha ushuru wa vizimba au meza kuwa Sh. 4,000 alisema kuwa yeye alikuwa safarini na hajui sababu za wao kufanya vurugu hizo.

Alisema ili kutoa majibu sahihi ni lazima afike katika eneo hilo la soko ndipo atatoa ufafanuzi.

Alisema: "Siwezi kuongea chochote nilikuwa nimesafiri, hivyo sijui sababu kamili za wao kufanya hivyo na ukiniuliza siwezi kujibu subiri nije huko ndio niweze kuongelea hilo".

# Ofisa Tarafa aokoa ekari za msitu zilizovamiwa na wakulima

**Na Dege Masoli,** KILINDI

EKARI zaidi ya 20 za Msitu wa Pagwi zilizovamiwa na wakulima, kufyeka na kukata miti kinyume na taratibu zimerejeshwa karika Serikali ya Kijiji cha Pagwi.

Pia, viongozi wa Kijiji hicho wameagizwa kuchukua hatua kali dhidi ya wahusika waliofanya uharibifu huo. Marufuku hiyo ilitolewa na Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Michael John baada ya kutembelea eneo hilo na kukuta uharibifu mkubwa unaotokana na watu kufyeka na kukata miti kwenye msitu huo.

Alifikia maamuzi hayo baada ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji hicho aliyoambatana nayo katika ziara yake hiyo ya siku moja kutokuwa na taarifa ya wafyekaji hao ikiwemo uhalali wao wa kuwepo kwenye msitu huo. Alieleza kuwa kutokana na Serikali ya Kijiji kutokuwa na taarifa ya kazi inayoendelea hapo amesimamisha shughuli zote na watu hao, kwamba wasakwe popote walipo na wachukuliwe hatua kali za kisheria.

"Kazi inayofanyika hapa ni uharibifu wa mazingira na kwakuwa Serikali ya Kijiji hamna maelezo kuhusiana na ufyekaji na ukataji huu wa miti, kuanzia sasa nasimamisha uendelezwaji wa eneo hili na wahusika wasakwe popote walipo waje kujibu hoja kwenu" alisisitiza John.

Awali, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Pagwi, Mussa Masali na wajumbe wake alimueleza Ofisa Tarafa huyo kuwa yeye na serikali yake haina maelezo ya namna watu hao walivyoyapata maeneo hayo na kwamba na wao wanashangaa kuwepo kwa hali hiyo. "Ninachofahamu ni kwamba kabla sijaingia madarakani eneo hili lilikuwa linamilikiwa na mkazi mmoja ninaemtambua kwa jina la Somon Elias, lakini eneo hili halikufanyiwa kazi kwa miaka mingi sana,"alieleza mwenyekiti huyo

Hata hivyo alidai kuwa mwaka huu Elias alifika ofisini na kutoa taarifa ya kuliuza kwa watu wengine na baada ya hapo ndipo kazi hiyo ikaanza kufanyika kwa kukata miti kwa ajiri ya kuchoma mkaa ili kujipatia kipato.

Mmoja wa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Siliwayo Mziwanda alieleza kuwa hafahamu chochote juu ya watu waliovamia msitu huo zaidi ya kubaini uwepo wa uharibifu huo katika eneo hilo baada ya kufanya ziara.

Mjumbe wa Serikali ya Kijiji hicho, Soda Kimilei alishangaa kutokea kwa ufyekaji huo, akidai kuwa licha ya kufuatilia kwa wahusika alipata majibu ya watu hao kupewa na uongozi ambao hata hivyo hakuutaja ni wa ngazi gani.





## Bil 1/- kumaliza kero ya maji vijiji vinne Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI zaidi ya 8,000 kutoka vijiji vya Mwalukwa, Bulambila, Kadoto na Ng'hama wilayani Shinyanga wanatarajia kuondokana na adha ya kutumia maji machafu, baada ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji katika vijiji hivyo kuanza kujengwa.

Mradi huo ambao unajumuisha tangi lenye lenye ujazo wa lita 100,000 pamoja na bomba kuu la maji tayari umewekewa jiwe la msingi na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme.

Wakati wa hafla hiyo, Mndeme aliwaagiza RUWASA kukamilisha mradi huo kwa wakati pamoja na kupanua mtandao wake wa maji.

Akizungumza juzi wakati wa uwekaji wa jiwe hilo Mndeme alisema serikali itaendelea kuhudumia wananchi na kutatua kero zao katika sekta mbalimbali kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya maendeleo.

"Nawapongeza RUWASA na Life Water International kwa kutekeleza mradi huu mkubwa kabisa uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni moja na ambao utatatua kero ya uhaba wa maji kwa wananchi zaidi elfu 8,000 ukiwa ni mtandao wenye urefu wa km 34, hakika ni furaha sana hata wananchi mmewasikia hapa," alisema Mndeme.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi watunze miundombinu hiyo ya maji ili ipate kuwahudumia kwa muda mrefu, huku akiwataka mafundi ambao wanajenga mradi huo wawe wazalendo na kutoiba vifaa vya ujenzi.

Katika hatua nyingine Mndeme alikagua ukarabati wa ujenzi wa bwawa la maji katika Kata ya Mwalukwa wilayani Shinyanga, ambalo litanufaisha wananchi zaidi ya 22,000.

Baadhi ya wananchi wilayani Shinyanga waliishukuru serikali kwa kuwatekeleza mradi huo pamoja na bwawa hilo la maji, wakisema ni miradi ambayo ni uhitaji mkubwa kwao, kwamba bila maji maisha hua magumu sana hasa maeneo hayo ya vijijini.

# Imani za kishirikina chanzo vifo wagonjwa kichaa cha mbwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UGONJWA wa kichaa cha mbwa umetajwa kuhusishwa na imani za kishirikina, hali ambayo imekuwa ikisababisha waathirika wa ugonjwa huo wilayani Kahama mkoani Shinyanga kufariki dunia, kunakosababishwa na kutofuatilia huduma za kitabibu hospitalini.

Imeelezwa kuwa wananchi hao wamekuwa wakipuuzia utaratibu wa kupatiwa chanjo ya ugonjwa huo hospitalini pindi wanapong'atwa na mbwa, badala yake wanakimbilia kwa waganga wa kienyeji kutibiwa kiasili, wakiamini wamelogwa hali ambayo imekuwa ikisababisha vifo.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Dk. Damiani Kilyenyi katika Maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa.

Alisema kuwa idadi kubwa ya wagonjwa hao wanafika hospitalini wakiwa wamechelewa baada ya huduma za kiasili kushindikana.

Dk. Kilyenyi alisema matatizo hayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara katika kata za Isagehe, Zongomela pamoja na Nyandekwa ambako wagonjwa na ndugu zao hushtuka na kufika hospitalini mgonjwa akiwa tayari ameanza kubweka kama mbwa.

"Mbwa asiyekuwa na chanjo akimng'ata binadamu ni rahisi kupata madhara ya kichaa cha mbwa na kisha kupoteza maisha.

Hii haina uhusiano kabisa na suala la ushirikina, hivyo tuwaombe waganga wa jadi kuacha tabia ya kuingilia fani za watu na badala yake wanapopata mgonjwa wa namna hiyo wamshauri kufika hospitalini haraka na siyo kukaa naye tu pasipo matibabu yoyote," alisema Dk. Kilyenyi.

Naye Ofisa Mifugo wa Kata ya Bulige, Halmashauri ya Msalala, Dk. David Sospiter alisema katika kata yake kuna watoto waling'atwa na mbwa kisha wazazi wao kuwakimbiza kwa mganga wa jadi wakiamini mbwa alikuwa ametumwa.

Alisema baada ya wiki moja Watoto hao walianza kubweka na kupoteza maisha.

Mratibu wa Chanjo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Mukola Vedasto aliwakumbusha wafugaji wenye mifugo kuhakikisha wanakuwa na utaratibu wa kuwapatia chanjo mbwa wao ili kudhibiti ugonjwa huo.

Alisema wamekuwa wakipokea wagonjwa watatu hadi watano kila siku ambao wameng'atwa na mbwa wenye kichaa na kwamba tang Januari hadi Agosti 16 mwaka huu wametoa chanjo kwa wagonjwa 218.




Ofisa mifugo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, Dk. James Nasari (kushoto), akitoa chanjo ya kichaa cha mbwa, wakati wa maadhimisho ya siku ya kichaa cha mbwa Duniani kwenye viwanja vya Magereza Kahama jana. Kulia ni mmliki wa mbwa huyo, Kashinje Dotto. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wanafunzi waomba elimu bima ya afya itolewe kwa wazazi

**Na Alphonce Kabilondi,** GEITA

BAADHI ya wanafunzi wa shule za sekondari mkoani Geita wameiomba serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kutoa elimu kwa wazazi na walezi ili kuona umuhimu wa kuwa na kadi za matibabu.

Wamesema hatua hiyo itawapunguzia wazazi wao gharama kubwa za matibabu wanapokuwa shuleni.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti katika Maonesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini mkoani hapa na kusema kuwa wamekuwa wakisumbuka kwa kukosa fedha za matibabu kutokana na kutokuwa na bima ya afya.

Mmoja wa wanafunzi hao, Joshua Juma alisema ni vyema wazazi na walezi wakapewa elimu ili kutambua umuhimu wa kadi za matibabu za mfuko wa bima ya afya pamoja na utaratibu mzima na faida zake ili waweze kuwakatia.

"Kuna kipindi niliugua nikiwa shuleni wazazi walitumia fedha nyingi kugharamia matibabu na shuleni hakukuwa na utaratibu wa bima bali malipo ya huduma za vipimo pekee ambayo haihusiani na matibabu makubwa,"alisema Juma

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Geita, Venance Raymond alisema kuwa mpango wa bima ya afya kwa wanafunzi utawasidia kuepukana na gharama za matibabu, hivyo kuutaka mfuko huo kuendelea kuimiza ipasavyo ili wazazi wawezo kuchangia kwa ajili ya watoto wao.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Geita, Elius Odhiambo alisema kuwa mfuko unaendelea kuboresha mazingira ya matibabu kwa wanafunzi kupitia mpango wa serikali wa bima ya watoto kwa gharama nafuu.

Alisema mfuko huo unaendelea kutoa kutoa elimu kupitia maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari juu ya umuhimu wa kuwaunganisha wanafunzi katika mpango wa pamoja wa bima ili kupunguza gharama za matibabu.




Ukurasa 13

Chifu Hangaya pangapangua iendelee



NGO yabuni mbinu ya waliotoka magerezani kuingia katika miradi ya kujimudu kiuchumi

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 29, 2023
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe

ULIVYO UCHUMI NA RUZUKU NCHINI

# Rais Dk. Samia akanyaga mkoani Lindi na ufafanuzi neema anayowaachia shambani

• Waziri Bashe afafanua ruzuku inavyopandikizwa, kumvusha mkulima

**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya majukumu ya kiserikali ambayo mzigo mkuu anaubeba rais katika nafasi yake, ni kwamba anatetea uwezeshaji wa kiuchumi katika ngazi ya kitaifa, ikishuka katika nafasi ya mtu mmoja mmoja.

Aina ya uwezeshaji huo hugusa nafasi ya ama moja kwa moja, au penye njia anakojitetea mtu kiuchumi katika maendeleo yake binafsi.

Na mara zote inapotokea uwekezaji, uwe katika nafasi ya kiserikali au wadau wengineo, mlengwa wa moja kwa moja huwa ni mtu wa kawaida.

Pia, mwananchi anapokabidhiwa neema hiyo ya maana, kuna kinachotajwa kuwe na 'thamani ya fedha' kwa maana ya kinachowekezwa, kifanane na lengo kumuwezesha mwananchi kuinuka kiuchumi, hata kimaendeleo.

Ndio dhana aliyotembea nayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye ziara ya wiki hii, hasa akazungumzia safari ya ruzuku na ukomo wake, unaomuachia neema mkulima.

Kimsingi, hadi sasa wakulima wa mikoa hiyo ya Kusini, wanafaidi ruzuku inayojionyesha katika mazao kama ya korosho na ufuta, kuinua nguvu yao katika uzalishaji na mapato, nchi nayo ikiinuka katika mapato ya jumla na fedha za kigeni.




Rais akizungumza wiki iliyopita, alipokuwa ziarani mkoa wa Lindi. **PICHA: MTANDAO.**

Hapo ndipo Rais Dk. Samia amelitolea ufafanuzi ziarani kwamba, hilo limefanyika kuwainua kiuchumi jamii hiyo na kasi ya uzalishaji wa mazao hayo ya kibiashara, ili inapofika hatua ya kundolewa ruzuku hiyo miaka michache ijayo, iwe katika sura ya ushindi kimaendeleo kwa ujumla na pato la taifa.

Wakati hilo linatumika katika mikoa ya Kusini mwa nchi, suala la ruzuku ya mbolea linatolewa pia katika mbolea mikoa yote kitaifa, ikiwa na sura hiyo hiyo ya kujijengea uwezeshaji katika uzalishaji chakula nchini.

Tangu kuingia madarakani, Tanzania katika eneo hilo la uzalishaji chakula iko vizuri na matokeo yanaonekana kufanya vizuri katika masoko ya jirani, hata baadhi ya nchi jirani zinazokabiliwa na upungufu wa chakula kutegemea nchini.

**MIRADI YA KUWEZESHWA**

Rais Dk. Samia amekuwa akihamasisha wakulima wa mikoa ya Kusini kuzalisha chakula kwa wingi na mazao mengine kuanza kuyalima kwa matumizi ya biashara kama mbaazi na ufuta.

Sambamba na hilo, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe naye katika hilo, anatoa hamasa kwa wakulima, akiwaeleza jitihada za serikali za kujenga kongani ya viwanda vya kubangua korosho, kwa dhamira ya kuongeza thamani ya zao hilo kibiashara kwa wakulima.

Anatamka serikali imepanga kuchimba mabwawa saba ya kuwezesha kilimo cha umwagiliaji, huku kwenye zao la korosho, Waziri Bashe anaeleza kuwa Wizara ya Kilimo imepokea maelekezo ya Rais Dk. Samia, kwamba katika mkoa wa Lindi, kutajengwa kiwanda cha kubangua korosho kama mkoa wa Mtwara.

**MICHE MIPYA**

Kuhusu mazao yanayolimwa kwenye mkoa wa Lindi, Waziri Bashe anayeambatana na Rais Dk. Samia ziarani Lindi wiki iliyopita, anasema mkoa utapatiwa miche 500,000 ya bure ya minazi ili wakulima waweze kupanda na kuanza kuvuna baada ya miaka minne ijayo.

Hapo Waziri Bashe anafafanua ni hatua itakayowasaidia wakulima kukidhi mahitaji ya nazi nchini, akiwa na ufafanuzi wa ziada: "Wizara ya Kilimo pia itatoa tani 30 za mbegu za ufuta kwa wakulima wa Lindi na tayari nimeshatoa maelekezo kwenye Bodi ya Korosho na Vyama vya Ushirika ili hilo lianze."

Ni kauli yake Bashe wastani wa zaidi ya wiki moja iliyopita, alipoambatana na Rais Dk. Samia, akifafanua kwamba Wizara ya Kilimo itagawa miche hiyo mwaka huu kutokana na uhitaji mkubwa wa nazi nchini.

"Mkoa wa Lindi wakulima wanazalisha mazao makuu manne makubwa yakiwa ni korosho, mbaazi, ufuta na mnazi, hivyo wakulima wa Lindi miche laki tano, kufuatia utafiti wa kina uliofanywa kwa miche ijulikanayo kama East African Tall, ambayo inavunwa kuanzia miaka minne baada ya kupandwa," anafafanua.

Kitaifa, mbali na ufuta unaozalishwa zaidi katika mikoa ya Kusini na kupewa uzito mkubwa, pia kuna korosho ambalo ni sehemu ya mazao saba ya kimkakati kitaifa.

Mengine yanayopatikana kwingineko nchini na kutiliwa mkazo ni; Tumbaku, Chai, Kahawa, Pamba, Katani na michikichi.

ends

UCHUMI

# NGO yabuni mbinu ya waliotoka magerezani kuingia katika miradi ya kujimudu kiuchumi

- Waanza na kinamama wanaojitambulisha wana ujuzi kibao
- DC Ilala awakaribisha milango yake iko wazi kuwapigania

**Na Beatrice Philemonn**

BAADA ya kuona wafungwa wengi wanaomaliza vifungo vyao katika magereza mbalimbali nchini na kurudi uraiani, wanakabiliwa na changamoto za kimaisha, hivi sasa baadhi ya wadau wamekuja na mkakati maalumu kuwakimu.

Kimsingi, magumu hayo yanatajwa ni katika maeneo kama vile msongo wa mawazo, afya ya akili yakiwa ni zao la ugumu wa maisha, ukosefu wa kipato, fedha za matibabu, kunyanyapaliwa na kunyimwa baadhi ya huduma za kijamii.

Sasa kunaelezwa, baadhi ya wadau wamekuja na mkakati kuwapatia elimu ya ujasiriamali na masuala mengine kwa wanawake, kwa waliomaliza vifungo au kuachiliwa kutoka magerezani, ili washiriki katika shughuli binafsi za uchumi na kijamii.

Lengo kuu la mkakati wanalitaja ni kuwasaidia kufanya shughuli za maendeleo kama vile kuanzisha miradi ya kujiajiri na kujiongezea kipato, kujitegemea kiuchumi, kuwapa matumaini mapya kimaisha, kusaidia familia zao, kuwapa ujasiri uanowaepusha kufanya makosa ya kijinai yanayowarudisha magerezani.

Akizungumza na Nipashe, Lucas Mwimo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali linaloitwa Tanzania Prisoners Hope Foundation (TPHP), mdau wa kusaidia wafungwa walioachiwa, anasema shirika lake limeamua kuja na mkakati huo, kuwaepusha kufanya makosa ya kijinai tena.

Hadi sasa jumla ya wanawake 33 waliomaliza vifungo kutoka magereza ya Dar es Salaam, wamepata elimu ya ujasiriamali na haki zao katika jamii.

Anataja hiyo ni baada ya kifungo, wakipata ushauri nasaha na kunolewa katika stadi za usimamizi wa fedha, jinsi ya kupata mikopo yenye riba nafuu kutoka taasisi mbalimbali za kifedha .



Mkufunzi kutoka kampuni ya Madeo Finance Limited, Kilasi Michael, akitoa elimu ya ujasiriamali kwa wanawake waliomaliza vifungo vyao magerezani na kurudi uraiani. **PICHA: BEATRECE PHILEMON.**

### KWANINI WANAWAKE?

Mwimo anasema wameamua kuwachagua wanawake, kwa sababu ndiyo wanaopata changamoto zaidi kuliko wanaume, hivyo wanataka kuwapa ushauri, pia moyo wakiwatafutia wadau wa kuwapatia mitaji kuanzisha shughuli za kiuchumi.

Anasema, pia watu hao wanaporudi katika maisha ya kawaida, kuna kawaida ya umma unawanyanyapaa matokeo yake, wanakabiliwa na tatizo la afya akili, kutokana na ugumu wa maisha unaowakabili.

Mkurugenzi huyo anafafanua, inapotokea mfungwa huyo aliyeachiwa, anapopatiwa elimu sahihi ya ujasiriamali, anakuwa na uwezo wa kuanzisha miradi ya kijasiriamali, hata wakajiepusha na mazingira ya kurudia tena makosa ya awali.

### WATAALAMU WA MAFUNZO

Ni mafunzo yaliyotolewa na waatalamu kutoka kampuni mbalimbali, chini ya kivuli cha shirika lisilo la kiserikali linaloitwa Women Fund Tanzania Trust (WFTT) na yakihudhuriwa na maofisa ustawi wa jamii, viongozi wa magereza, Mkuu wa Gereza la Wanawake Segerea na wawakilishi kutoka WFTT.

"Tunashukuru shirika la WFTT kwa kutupatia fedha ambazo zimetusaidia kukutana na wanawake hawa na kuwapa elimu ya ujasiriamali kujua changamoto zao na vitu wanavyohitaji kutoka serikalini na jamii kwa ujumla," anasema Mkurugenzi wa Tanzania Prisoners Hope Foundation, Lucas Mwimo.

Anasema, hivi sasa shirika hilo linatafuta wafadhili wengine wa kuwasaidia kupata fedha zitakazowezesha kutoa mitaji midogo kwa wanaotoka jela kuanzisha maisha mapya.

Mwimo anataja hilo lina tafsiri pana, kuanzia kunahitajika walau Sh. milioni 50, za kufanikisha lengo hilo

### WAWASHAURI WAFUNGWA

Ana mapendekezo kwa wafungwa waliokaa muda mrefu magerezani na kupata ujuzi walikokuwa, pale wanapomaliza vifungo vyao, ni vyema serikali au halmashauri za serikali za mitaa wanakoishi ziwapatie angalau mitaji midogo ya kuanzisha ili wakatumie ujuzi walioupata vifungoni.

Wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla, pia wanatajwa wawajibike kuunga mkono juhudi zinazofanywa na TPHF katika kutatua changamoto zinazowakabili ndugu zetu wanaomaliza vifungo vyao.

> **"Tukiungana kwa pamoja tutawafanya wenzetu hawa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo na hivyo kuondoa uwezekano wa kurudia makosa ya kijinai," anasema.**

"Tukiungana kwa pamoja tutawafanya wenzetu hawa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo na hivyo kuondoa uwezekano wa kurudia makosa ya kijinai," anasema.

Pia, anasema hadi sasa kitaifa hakuna sheria inayowafanya wanaotoka magerezani, kuungana na familia zao pamoja au jamii kiurahisi.

"Tunapendekeza kuwapo sheria hiyo au kanuni ndogo ndogo kwenye halmashauri zetu, ili kusiwapo tabia ya kuwanyanyapaa, kwani hawa bado ni wanadamu wanaostahili kupata huduma zote za kijamii na hawapaswi kuendelea kuhukumiwa au kunyooshewa vidole na jamii," anaeleza.

Pia, katika hilo anaomba wanawake waliomaliza vifungo na wale waliotoka mahabusu, kuunda umoja wao ili sauti zao zisikike kirahisi mbele ya wadau wengine, hata wakasaidiwa kirahisi.

"Mnaweza kuanza na kundi hili dogo mkawa na viongozi wenu ili muweze kusaidia kiurahisi. Mara wadau wanapojitokeza kutoa misaada na sisi kama TPHF, tunaendelea kuomba misaada kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi na mara itakapopatikana mtakuwa watu wa kwanza," anasema mkurugenzi huyo.

### WALIOMALIZA MAFUNZO

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wenzake, Veronica Ndunguru, anaunga mkono wazo hilo kutoka shirika lisilo la kiserikali akilitaja 'linawakumbuka', pia kuwapa elimu ya ujasiriamali.

Veronica anaeleza: "Mafunzo yamefungua akili zetu, elimu tuliyoipata imetugusa na tutakwenda kuifanyia kazi na hatimaye kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii."

Anaitaja kuwa ni hatua kubwa sana, kwa sababu tangu watoke gerezani, hakuna taasisi au shirika lililowahi kufanya jitihada kama hizo za sasa, kuwakutanisha kwa lengo la kujua changamoto zao na kazi wanazofanya

"Tumefurahi kukutana na kutoa changamoto zetu tunazokutana nazo uraiani, ili serikali na wadau wengine waweze kuzifahamu na hatimaye waone jinsi gani wanaweza kutusaidia kutatua changamoto hizo," anasema.

### CHANGAMOTO ZA URAIANI

Veronica anataja changamoto ya kwanza, ni hali ya kunyooshewa kidole na jamii, kutokana na makosa yaliyofanyika siku za nyuma, hivyo wananyanyapaliwa na kunyimwa baadhi ya huduma za kijamii, kama vile nyumba za kupanga na misaada ya kujikimu.

Pia, anataja msongo wa mawazo na afya ya akili inayowakabili, kutokana na maisha yao uraiani kuwa magumu, ukosefu wa kipato na fedha za matibabu na wengi wao hawana bima ya afya.

Ni hali inayofanya kuibuka kwa magonjwa mengine kwa wengi, ikiwamo shinikizo la damu, kisukari na magonjwa ya moyo.

"Tunaomba sana taasisi ya TPHF ishirikiane na wadau wengine kutupatia semina za afya ya akili mara kwa mara kwani kutokana na msongo wa mawazo na afya ya akili, baadhi yetu hufikia uamuzi wa kutaka kujiua na wengine kuingia kwenye ulevi wa kupindukia na hatimaye kupoteza matumaini ya kuishi na hata wengine kurudia kufanya makosa ya kijinai," anasema.

Changamoto ya tatu: anaitaja ni kukosa mitaji ya kuanzisha shughuli za ujasiriamali, kwani wengi wao hawakopesheki kwenye taasisi za fedha, maana hawana dhamana zozote.

Hapo wanazitaja ni changamoto zinazowafanya wanawake waliotumikia vifungo na kumaliza, wanakuwa na mchango mdogo kiuchumi katika familia, ilhali baadhi yao wana ujuzi walioupata magerezani.

"Mbali na hilo, kutokana na tatizo la ajira na ukosefu wa mitaji ya kujiajiri wenyewe miongoni mwetu, hatunufaiki na ujuzi huo tulioupata tukiwa gerezani na mfano mzuri kuna baadhi yetu ni mafundi wa kushona na kudarizi mashuka.

"Tunaamini ofisi ya TPHF ina uwezo wa kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hili kwa kutoa mikopo midogo hata mikubwa ili tujiajiri wenyewe na hatimaye tusirudie makosa ya awali yaliyotupelekea tukapata adhabu ya vifungo," anasema.

Katika hilo anasisitiza jamii ielimishwe kuwapokea vizuri wanapotoka magerezani na wasihukumiwe kutokana na makosa waliyofanya siku za nyuma.

"Sisi sio wahalifu tena, bali ni raia wa kawaida wanaostahili kupewa haki zetu za msingi na kuthaminiwa na jamii kama Mungu anavyotuthamini na kutusamehe dhambi zetu pale tunapotubu na kuomba msamaha," anatamka.

Pia wanaiomba serikali, taasisi binafsi, wadau washirikiane kutoa elimu kupitia semina na warsha kuhusu wajibu wa raia kwa vijana mtaani na wanafunzi shuleni, ili kusaidia kujenga maadili ya jumla katika jamii, wasiangukie janga la kuingia magerezani.

### MKUU WA WILAYA YA ILALA

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, anayashukuru mashirika ya WFTT na TPHP, akiwa na maoni yake: "Naomba walimu na wadau wengine waone jinsi ya kufundisha watu hawa akili hisia (Emotional Intelligence), ili wanapokutana na changamoto uraiani wajue jinsi ya kutoa maamuzi, pia changamoto hizo zisiwapeleke kwenye vitu potofu kwa maana nyingine wawe na 'positive attitude' (hisia chanya) na hii itasaidia wawe watu wengine."

Lingine, Mpogolo anaziasa jamii zao kuacha kuwanyanyapaa katika mwanzo huo wa maisha mapya katika jamii, akitaja wilaya yake ipo tayari kuwasaidia kupata mitaji.

"Mnaweza kujiunga katika kikundi na kuomba mikopo, tunao wataalamu ambao watawasaida jinsi ya kuandika maombi ya mikopo. Mkiwa wamoja, maofisa mikopo wetu watawapatia mikopo na serikali itawasaidia," anasema.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Chifu Hangaya hiyo pangapangua iendelee






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

JUMANNE, yaani juzi tu, Chifu Hangaya wakati akiapisha wateule wake, alilalamika kukosekana kwa taarifa za kutosha kumwezesha kuteua na kutengua na kuhimiza zimfikie mapema ili aweze kutekeleza vema majukumu yake.

Na pengine ndiyo sababu katika uteuzi wake hivi karibuni, alijikuta akifanya mabadiliko kwa muda mfupi kwa Maharage Chande na Peter Ulanga kuhusu nani aendeshe Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL).

Alishampeleka Maharage TTCL, kwa kumtoa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), akiamini kutokana na ubobezi wake katika masuala ya kidijitali basi mambo yatakwenda bulbul.

Lakini kumbe taarifa zilichelewa njiani kumfikia, zikimwonyesha kuwa Maharage ana unasaba fulani wa kibiashara na TTCL, hivyo kumweka pale, kungeweza kumrahisishia masuala yake ya hulua.

Akashtukia jambo na akamvuta shati na kumpeleka Shirika la Posta kuwa Posta Masta Mkuu, kwani na huko udijitali unahitajika sana, hasa pale Chifu Hangaya alipobaini kuwa kumbe Posta yetu inatamba miongoni mwa zingine duniani.

Ulanga ambaye alishatangaziwa kuwa atapangiwa kibarua kingine, wafanyakazi wake TTCL wakawa wamebaki kugugumia kwa uchungu wasiwe na la kufanya, kwa sababu jembe lao lilishawekwa pembeni.

Chifu Hangaya akaja kuambiwa kuwa kama si Ulanga pale TTCL, haki ya nani mambo yasingekuwa kama yalivyo, akajilaumu kwa kutojua hayo na kumrejesha haraka. Nasikia watumishi hao wakakimbilia nyumba za ibada kumshukuru Muumba.

Baada ya kusikia mabadiliko hayo ya haraka, mkazi mmoja wa Tegeta akanipigia simu na kumwunga mkono Chifu Hangaya, kwa kulalamikia watu kuchelewesha au kutotoa kabisa taarifa mpaka kumpotosha. Watoa taarifa sijui wanafikiria nini?

Lakini, mkazi huyo pamoja na kumshukuru Chifu Hangaya kwa maoni yake hayo, akaniuliza hivi kama kweli Maharage ana dili fulani la kibiashara na TTCL, kwani hawezi kuwasiliana tu na Ulanga akamwekea masuala muswano, kwa kuwa wote ni mabosi wakuu wanaolingana?

Nikamjibu inawezekana wakafichiana na kusaidiana mengine, lakini Chifu Hangaya akiwamulika huo ni kwamba watapoteza vibarua vyao? Eti akanijibu hayo mambo kwa Wabongo yalishapitwa na wakati, ni chukua chako mapema.

Akaongeza, eti kwamba wanajua watahamishiwa kwingine tu na hivyo hawatapoteza, kwani ukishaingia kutoka ni mbinde, ili mradi unapiga mzigo, haya mengine hujipeleka yenyewe. Alitaka nimwamini kuwa ni mzunguko wa kubadilisha vijiti, hakuna kutoka!

Sikutaka kumbishia, kwa sababu kila mtu na mawazo yake, kila mtu na imani yake, hivyo anavyoona ndivyo, ingawa duniani yote yawezekana, kwamba kuna watu wakishaingia kwenye mfumo kutoka ni mbinde, tumewasikia miaka nenda rudi na bado tunawaona.

Wakati naongea na mgeni wangu huyu, ghafla akaja jirani naye wanguwangu bila kujua tunazungumzia nini, akabwatuka tu akisema Rais angewaondoa tu hao, badala ya kuwabadili nafasi, ili wapishe wengine. Kumbe alikuwa na hasira, eti jokofu lake usiku wa jana liliungua baada ya umeme kurudi na nguvu.

Sasa kumbe hasira zake akawa amezielekeza kwa Maharage, akisema ni chanzo cha umeme kukatikatika, eti kwa nini enzi zile kabla yake mambo hayakuwa hivi. Nikamjibu nikimkariri Chifu Hangaya kuwa tatizo si Maharage ni sisi sote. Akanitazama kwa hasira.

Nikamwambia nikimkariri tena Chifu Hangaya, kwamba kumbe mitambo ilikuwa ikiendeshwa ikiwa chakavu na hivyo sasa tunakula jeuri yetu ya kutoifanyia ukarabati, sambamba na maji kupungua kwenye mabwawa.

Nikamfahamisha kuwa yale mabwawa yetu yaliyokuwa na maji, kulitokea mabadiliko ya tabianchi, pia mabadiliko ya tabiamtu na hivyo maji kwisha kwenye mabwawa kwa kukauka na mengine kumwagika yalipotishia kupasua kuta za mabwawa. Nikawaza Bwawa la Nyerere itakuwaje!

Sasa tusubiri kuona kama mambo yatakuwa muswano huko walikopelekwa viongozi wapya na kama kweli walichomwahidi Chifu Hangaya, ndicho watakifanya ili tuondokane na kadhia hii, hususan ya umeme, pia binamuye, maji ambako nako ni msiba.

Ndugu yangu Nyamuhanga kapewa miezi sita kuhakikisha hakuna katika ya umeme, kama namwona vile, ingawa naamini atapambana na zimwi hili hata kulishinda, ili yasijirudie ya kufurahisha wauza kaangavuke pale Kariakoo.

Lakini, tufanye yoote hayo na tukiyamaliza hayo ya upungufu wa umeme aka mgawo, turudi kwa hayo mengine, tukikumbuka kuwa mwakani na mwaka keshokutwa kuna madebe yatatuhusu. Inshallah!

MKURUGENZI WA TGNP - LIUNDI:

# Mfumo dume katika uchumi leo nyumbani, tabu imemgeukia baba

## • Aibu, mazoea yawatwisha mizigo kimyakimya

**Na Beatrice Moses**

KATIKA jamii kuna mada mfumo dume unaoatajwa kuwa hali ya mwanaume kuanzia kwenye ngazi ya familia ya jamii, kwa ujumla kuwa ndio wenye maamuzi pekee.

Awali ilitawala imani, kwamba mfumo dume unaaminika kuwakandamiza wanawake pekee ndani ya jamii, lakini sasa umebadilika, zikimea ishara kuwa sasa inawaathiri wanaume zaidi kiuchumi na hasa kwa wenye kipato cha kati na chini .

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anautakia ni mfumo unaowajengea wanaume fikra za kupambana binafsi, kutafuta kipato na kutunza familia, hata akikwama kwa kutawaliwa na hofu za kumshirikisha majukumu mkewe, hata kama kamzidi kipato.

"Mfumo dume umewajengea hofu baadhi ya wanaume kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa, ukilinganisha na ushiriki wa wanawake. Wanaume wanapambana kivyao tu, huku wakiwa wametawaliwa na hofu na kupoteza heshima ya uongozi ndani ya familia, kwa kuwa wana kipato kidogo," anasema Liundi.

Liundi anasema, kutokana na kampeni ya kuwakomboa wanawake, sasa wengi wana elimu, hivyo wapo walioajiriwa na wanalipwa vizuri.



Walivyo wanafamilia kwenye mkusanyiko wao. **PICHA: MTANDAO.**

Pia anataja kuwapo kwa sababu ya mfumo dume, kinamama huwa hawabanwi kugharamia majukumu ndani ya familia, hivyo inabaki kuwa wajibu wa mwanaume zaidi.

Mama huyo anasema kuwa, mwamko wa wanawake kushiriki kwenye kujitafutia kipato ni mkubwa, hivyo wapo wenye uhakika wa kipato kulingana na shughuli wanazofanya, ikiwamo ujasiriamali, hivyo wanaweza kuhudumia familia zao.

"Novemba saba hadi 10 mwaka 2023, TGNP tunatarajia kufanya Tamasha la 15 la Kijinsia Dar es Salaam, linalotarajiwa kuhudhuriwa na watu zaidi ya 1500, watakaotoka nchi mbalimbali wa hapa nchini na kutoka nje ya nchi, hapo wanatarajia kujadili mambo kadhaa, ikiwamo ya usawa wa kijinsia," anasema.

Analitaja kuwa tamasha litakalokuwa jukwaa linafaa kuwa chachu ya kuleta mabadiliko kwenye suala la usawa wa kijinsia, ikiwamo kupambana na mfumo dume ndani ya jamii na kusaidia kuleta maendeleo ya kiuchumi kwenye familia na jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu Liundi, TGNP inaendelea na jukumu lake la kuelimisha jamii na kufanya harakati zake za kuhamasisha usawa na tayari kuna mafanikio kadhaa, ikiwamo ya kisheria wanawake walioajiriwa kupata likizo ya uzazi (siku 84), pia wanaume waliooa kupata siku (tatu) za mapumziko ya uzazi.

"Tumepambania hiyo, japo hatuna uhakika likizo ya uzazi ni siku chache anazopewa mume, mke wake anapojifungua, kuwa anazitumia ipasavyo. Lakini, tunashukuru ilifanikiwa kampeni yetu, maana awali mwanaume alinyimwa mapumziko," anasema.

**WAHUSIKA WAFUNGUKA**

Mkazi wa Dar es Salaam, Antidius Karumuna, anasema kuwa tabia ya kukosekana uwazi, ni sehemu inayowatesa baadhi ya wanaume, kwa kuwa hata wanapokabiliana na matatizo, bado wanajaribu kuyatatua kwa njia binafsi wanayoijua wao.

"Hali hii inatokana na imani tuliyojengewa wanaume, ni kupambana kutekeleza majukumu yanayokuhusu kulingana na uwezo ulionao na siyo kutangaza, au kulia lia," anafafanua.

Miongoni mwa majukumu aliyo nayo mwanaume ni pamoja na kuhakikisha wanafamilia wanapata mahitaji yote muhimu, ikiwamo elimu kwa watoto, inakuhusisha mahitaji kama vile ada, sare za shule na vifaa vinginevyo vinavyohitajika kulingana na shule anayosoma mtoto.

Mahitaji mengine yanatajwa, ni chakula, hapo akipaswa kuhakikisha familia inapata milo mitatu ya muhimu, ambayo ni asubuhi, mchana na usiku, pia kugharamia afya, mavazi na mahitaji mengine ya lazima.

Mdau Karumuna, anatetea mazingira hayo kwamba ndani ya familia, majukumu ya mwanaume yanatambulika, ikiwamo kwa mujibu wa sheria.

Anataja utamaduni au mazoea, mara zote mahitaji ya mtoto yanabaki kuwa yake mwanaume, huku ikiangaliwa upande wa pili hitaji la mwanamama kuwa mambo madogo, akichukuliwa kwamba uwezo wake ni wa chini, hivyo Karumuna anasisitiza haja ya elimu kutolewa kwa jamii kuleta mabadiliko.

"Kuondoa dhana hiyo ni suala la elimu kwa familia nzima kutambua kwamba, matatizo yanapoikabili familia, ni vyema kushirikiana kusaka ufumbuzi kwa pamoja," anasema.

**SHERIA YA NDOA**

Katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inabainisha mambo kadhaa kuhusu maisha yao wanandoa, ikiwamo majukumu yanayowakabili.

Sheria hiyo ina vifungu vinavyoainisha wajibu kwa mume kumtunza mke wake, kwa kumpa mahitaji yote muhimu katika maisha, kama vile mavazi, chakula na malazi kulingana na uwezo wake.

Pia inamtaja mke anakuwa na jukumu hilo, pale mume anashindwa kutunza familia, kwa sababu kama za ugonjwa, hasa wa kiakili na ulemavu.

Aidha, Sheria ya Ndoa, inazuia nafasi ya unyanyasaji wa kimwili kati ya wanandoa na kuacha aina nyingine za unyanyasaji ambazo ni za kihisia, kisaikolojia, kingono na kiuchumi.

Ikirejewa Kitabu cha Mafunzo ya Jinsia Mwongozo kilichotolewa na mhusika 'ViAgroforestry' cha mwaka 2018, kina vipengele vinavyoainisha nafasi ya kuwapo mafunzo ya ujumuishaji usawa wa jinsia.

Katika hilo, kunabainisha ujumuishaji wa usawa wa jinsia, kwamba ni mchakato wa kuhakiki vidokezo kwa wanawake na wanaume, kwa mpango kazi wowote, ikimjumuisha sheria, sera au programu, katika eneo au ngazi nyinginezo.

"Ni mkakati wa kufanya changamoto na uzoefu wa wanawake pamoja na wanaume kuwa sehemu muhimu ya kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini sera na miradi au/programu katika maeneo yote kisiasa, kiuchumi na kijamii, inabainishwa.

Ufafanuzi unaohitimisha unasema: "Wanawake na wanaume waweze kufaidi kwa usawa na kufanya ukosefu wa usawa usiendelee kutamalaki."






Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba (katikati), akiwa pamoja na Mkurugenzi wa huduma kwa mlipa kodi wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Richard Kayombo (kulia), wakiangalia jinsi ya kuskani kinywaji kwa njia ya mfumo wa kielektroniki (ETS), unaotolewa na kampuni ya SICPA, ili kuhakiki stempu na kuhakikisha kinywaji ni salama kwa matumizi ya binadamu katika kampeni iitwayo "Hakiki Stempu, Linda Afya yako", jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ramani kuzitambua NGOs kuzinduliwa ili kuongeza uwazi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuzindua ramani ya kidijitali ya utambuzi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima alitoa taarifa hiyo jana jijini hapa wakati akizungumza kuhusu uzinduzi huo na Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Alisema msingi wa kujengwa kwa ramani hiyo unatokana na maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan na kusisitizwa na Waziri mwenye dhamana kupitia kikao kazi cha wadau wanaotekeleza afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kilichofanyika Februari 26, 2022.

Alisema ramani hiyo itawezesha mashirika yasiyo ya kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ili kuleta maendeleo endelevu nchini na mchango wake kuonekana bayana katika maendeleo ya taifa.

"Hadi kufikia Septemba 22, mwaka huu jumla ya mashirika yaliyosajiliwa na kuwa hai ni 9,900 na kati ya hayo ya kimataifa ni 588, kitaifa ni 8,199, kimkoa ni 465 na kiwilaya ni 648," alisema.

Alifafanua kuwa maelekezo hayo yalitokana na changamoto ya kiutendaji iliyojadiliwa kuhusu baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali kutekeleza miradi na afua mbalimbali zinazofanana ndani ya eneo moja na kwa walengwa wa aina moja, hivyo kusababisha maeneo mengine kutofikiwa na huduma zitolewazo na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

"Wizara kwa kushirikiana na wadau iliamua kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuongeza ramani ya utambuzi wa mashirika haya kwa njia ya kidijitali," alisema.

Alibainisha kuwa ramani hii itasaidia wadau, taasisi za kiserikali, sekta binafsi na jamii kupata taarifa za mashirika hayo kwa urahisi mahali popote.

"Kimsingi ramani hii imejengwa na wataalam wetu wa ndani kutoka Idara ya Sosholojia na Anthropolojia na Idara ya Sayansi ya Kompyuta na Uhandisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)," alisema.

Alisema faida za kuwepo kwa ramani ya utambuzi wa mashirika kwa njia ya kidijitali ni pamoja na kujua mahali/ eneo shirika lilipo, kujua eneo la utekelezaji wa miradi ya mashirika , kujua afua zinazotekelezwa; kujua wanaufaika wa mradi na kujua ajira zilizotolewa na mashirika.

Alisema pia ni kuuliza na kupata majibu ya moja kwa moja, kujua fursa zilizopo, kujua mashirika yaliyokiuka vigezo vya usajili wake, kutambua mchango wa mashirika kupitia fedha za miradi, kujua idadi ya mashirika kwenye kila mkoa, wilaya na halmashauri na kujua miradi inayotekelezwa kwa wingi au uchache katika mikoa.

Katika hatua nyingine, alisema wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) ambalo ni mwamvuli wa mashirika hayo imeandaa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali litakalofanyika kuanzia Oktoba 3 hadi 5 jijini hapa.

Alisema mgeni rasmi katika jukwaa hilo anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, lengo likiwa ni kuimarisha uhusiano baina ya serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine pamoja na kutambua mchango wa mashirika hayo kwa maendeleo ya taifa.

Kaulimbiu ya jukwaa ni 'Mashirika yetu, maadili yetu, taifa letu' ambayo ilianza kufanyiwa kazi kwenye majukwaa ya mashirika yasiyo ya kiserikali ngazi ya mikoa.

# Wazazi wenye watoto vichwa vikubwa waiangukia serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha wazazi wa watoto wenye tatizo la vichwa vikubwa na mgongo wazi kimeiomba serikali pamoja na wadau wengine kuwasaidia kinamama waliotelekezwa na waume zao kutokana na kuzaa watoto wenye tatizo hilo.

Mkurugenzi wa chama hicho, Suma Mwaipopo, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kero mbalimbali zinazowakabili wazazi pamoja na watoto wenye tatizo nchini.

Alisema asilimia 25 ya kinamama wa watoto wenye tatizo hilo wametelekezwa na wanaume wao hali ambayo inachangia wengi kuwa na maisha magumu na kushindwa kuhudumia watoto hao.

"Wazazi ambao wanaishi na watoto wenye shida hii kwa kiasi kikubwa na wanawake ambao pia wengi wao wametelekezwa na waume zao baada ya kuzaa watoto wenye tatizo hili hivyo kusababisha kupitia maisha magumu na kushindwa kumudu gharama za matibabu"alisema Mwaipopo. Alisema kutokana na hali hiyo wanaiomba serikali pamoja na wadau wengine kukiwezesha chama hicho ili kiweze kusaidia watoto hao kupata matibabu ambayo ni mzigo mkubwa kwa wazazi kuzimudu.

"Matibabu kwa watoto hawa ni gharama sana na wazazi wengi wenye watoto hawa pia maisha yao ni duni kutokana na kutelekezwa na waume zao, hivyo kama chama chetu kitawezesha kitakuwa na uwezo wa kuwahudumia kwenye matibabu," alisema.

Kadhalika, alisema katika kukabilina na hali hiyo chama hicho kimefanya jitihada mbalimbali za kusaidia wazazi na watoto wenye shida hiyo ambapo hadi sasa watoto 12,000 wamepatiwa msaada.

Pia, alisema chama hicho kimejenga nyumba jijini Dar es Saalam ambayo inatumia kama nyumba ya matumaini kwa ajili ya kuhuduma wazazi wanaotoka mikoa mbalimbali wanaokwenda kusubiri huduma za matibabu.

Alisema: "Chama chetu hivi sasa kinafanya kazi katika mikoa 11 na kinawanachama 7,000, lengo letu ni kusaidia watoto hawa kwa kuwapatia matibabu ikiwemo kutoa bima za afya lakini pia nyumba hii inapunguzia gharama.

"Tatizo hili na kichwa kikubwa na mgogo wazi wataalam wanasema linatokana na upungufu wa madini ya folic acid kwa hiyo tunaelimisha jamii ili kupunguza tatizo hilo na kuzaa kwa watoto wenye shida hii" alisema.

Aidha, alisema lengo la chama hicho ni kuhudumia watoto 1,500 kila mwaka mwenye shida hiyo lakini kutokana na ufinyu wa bajeti mwaka jana wamehudumia watoto 1,230.

# Bashungwa: Barabara App suluhisho ubovu wa miundombinu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amewataka wananchi kutoa taarifa za hali ya barabara nchini kupitia mfumo wa kielektroniki wa 'Barabara App' ili hatua za haraka kwa barabara zinazohitaji matengenezo ziweze kuchukuliwa.

Alitaja miongoni mwa taarifa hizo ikiwamo barabara kujifunga, daraja au kalvati kubomoka/ kuzolewa na mafuriko, mashimo hatarishi barabarani, kazi kufanyika chini ya kiwango, mitaro kuziba na hujuma zozote zinazofanyika katika miundombinu ya barabara.

Waziri Bashungwa aliyasema hayo jijini hapa wakati akihitimisha ziara yake katika Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), pamoja na mambo mengine alipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya bodi hiyo.

Alisema kupitia mfumo huo, watumiaji wa barabara wanaweza kushiriki katika kusimamia miundombinu ya barabara katika maeneo wanayoishi au kupita kwa kutuma taarifa muhimu za hali ya barabara katika Bodi ya Mfuko wa Barabara, ambayo itawasilisha mahala husika katika Wakala ya Barabara Nchini (TANROADS) na Wakala ya Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

"Niwaombe Watanzania kutumia mfumo huu unaomwezesha mwananchi kutoa taarifa ya hali ya miundombinu ya barabara yenye changamoto au hujuma yoyote maeneo anayoishi", alifafanua Bashungwa.

Bashungwa aliongeza kuwa lengo la kuwa na mfumo huo ni kuipunguzia Serikali gharama kubwa za matengenezo ambayo ingeia kutokana na uchelewaji wa matengenezo hayo.

Aidha, Bashungwa alisema kuwa serikali imejipanga vyema kuhakikisha TANROADS inayosimamia barabara kuu na za mikoa na ile ya TARURA, inayosimamia barabara za halmashauri/ wilaya wanajipambanua zaidi katika kuhudumia barabara zote nchini.

Aliwataka Watanzania kuwa na imani na taasisi hizo katika kuhudumia na kusimamia mtandao barabara nchini kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu yao.

"Ningependa kuwajulisha Watanzania kuwa huko nyuma kulikuwa na maombi makubwa ya barabara ambazo zipo kwenye wilaya zetu ili zipandishwe hadhi kuja TANROADS, lakini hivi sasa hilo hitaji ni kama limeisha kwasababu TARURA imeshajengewa uwezo na kuimarishwa mfuko wake,"alisema Bashungwa.

Kaimu Mtendaji wa RFB, Rashid Kalimbaga, alieleza kuwa mbali na mfumo wa kieletroniki wa kufuatilia barabara bodi imeimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuzuia matumizi mabaya ya fedha.

Alisema kuimarika kwa mifumo hiyo kutaziba mianya ya uvujaji wa mapato pamoja na uchakachuaji katika ujenzi na matengenezo ya barabara.





Baadhi ya vijana watunza kumbukumbu, wataalamu wa tehama na maofisa tathimini na ufuatiliaji walioajiriwa na serikali kwa ajili ya kufanya kazi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mkoani Mbeya, wakipatiwa mafunzo ya kazi kabla ya kupelekwa kwenye vituo vya kazi walivyopangiwa, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yaanza uboreshaji taarifa wanaoishi na VVU

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa mapambano ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi wameanza kuboresha taarifa za watu wanaoishi na ugonjwa huo katika mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Hivyo vijana 324 wataajiriwa kwa lengo la kuwahudumia walengwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mchakato wa kuwaajiri vijana hao umefanywa na Taasisi ya Benjamin Mkapa ambayo ndiyo iliyoingia mkataba na serikali kushughulikia masuala ya rasilimali watu kwenye sekta ya afya.

Akizungumza wakati wa kutoa mafunzo kwa vijana hao kabla ya kuingia kazini, Ofis Rasilimali Watu wa Taafisisi ya Benjamin Mkapa, Violet Mlay alisema ajira za vijana hao zitakuwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya.

Alisema vijana hao wamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni watunza kumbukumbu, maofisa TEHAMA na maofisa tathimini na ufuatiliaji na kwamba mikoa inayolengwa ni Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

Alisema Mkoa wa Mbeya utapata watumishi 152, Songwe 61, Rukwa 61 na Katavi watumishi 52 na kwamba watagawanywa kwenye zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufani za mikoa na Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

"Lengo la serikali na wadau akiwemo HJFMRI ni kuhakikisha huduma zinaboreshwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, utaratibu huu unafanyika ni kwa mara ya pili baada ya ule wa awali ulioanza mwaka juzi kukamilika," alisema Violet.

Akifungua mafunzo kwa vijana watakaofanya kazi mkoani Mbeya, Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Raslimali Watu wa Mkoa huo, Donald Bombo aliwataka vijana hao kwenda kufanya kazi kwa uadilifu ili kuisaidia serikali kupata matokeo mazuri.

Aliwataka kuhakikisha watunza siri za wagonjwa wanaowahudumia kwenye vituo vya kazi pamoja na kutunza siri za ofisi ili kuepuka kusababisha matatizo ikiwemo migogoro kwenye maeneo yao ya kazi.

Aliwataka kufanya kazi kwa kushirikiana na watumishi wengine watakaowakuta kwenye vituo vya kazi ili kuongeza ufanisi na kwamba watakaofanya kazi hiyo vizuri wanaweza wakaendelea kwa awamu nyingine.

"Lakini pia hakikisheni mnawasiliana vizuri kwenye vituo vyenu vya kazi, vaeni mavazi ambayo yana staha na muwaheshimu watu wote mtakaofanya nao kazi kwenye maeneo yenu," alisema Bombo.

Baadhi ya vijana waliopata ajira hizo waliahidi kwenda kufanya kazi kwa bidii na kwa kufuata miongozo mbalimbali ili kufikia malengo ambayo serikali na wadau wanayahitaji.

Mmoja wa vijana hao, Jane Mwasumbi ambaye ni mtaalamu wa takwimu alisema atahakikisha anatumia maarifa aliyoyapata kuhakikisha anafanya kazi kwa uadilifu akidai kuwa kundi wanalokwenda kufanya nalo kazi ni kundi linalohitaji umakini mkubwa.

# Wakulima wa mahindi walia na walanguzi, waomba serikali

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

BAADA ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kusitisha ununuzi wa mahindi kwa wakulima wilayani Ludewa katika Mkoa wa Njombe kwa muda wa wiki tatu, wakulima hao wameiomba serikali kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuendelea na ununuzi ili kuondokana na walanguzi.

Wakulima hao waliwasilisha ombi hilo mbele ya Kamati ya Siasa ya CCM mkoani Njombe walipofanya ziara wilayani humo ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya chama hicho katika miradi mbalimbali.

Mmoja wa wakulima hao, Antony Haule na Adelina Mtega walisema kuwa wakati NFRA wakinunua mahindi hayo iliwasaidia kuwaepusha na walanguzi waliokuwa wanapita mitaani kununua mahindi hayo kwa gharama ndogo.

Haule alisema serikali iliongeza bei ya ununuzi kutoka bei ya awali ya Sh. 400 hadi Sh. 500 kwa kilo na kufikia shilingi 860 hadi shilingi 900 kitu ambacho kilileta hamasa kwa wakulima hao kupeleka mahindi yao kwaajili ya kuyauza NFRA lakini toka zoezi lisitishwe wamejikuta wakibakiwa na mahindi mengi nyumbani na kuishia kuyauza tena kwa walanguzi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Njombe, Julius Peter, alisema serikali ya CCM inayoongozwa na Mwenyekiti wake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ipo kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali za wananchi hivyo changamoto hiyo wataifikisha mahali husika ili iweze kupatiwa ufumbuzi na kuwasaidia wakulima.

"Suala hili tutalifikisha kwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ili aweze kulifanyia kazi kwani chama chetu ni sikivu na kimelenga kuwaletea maendeleo wananchi wake, hivyo tutahakikisha suala hili linafanyiwa kazi"alisema Peter.

Nao wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa huo, Theopista Mhagama pamoja na Emmanuel Mgaya waliwataka wananchi kuendelea kujenga imani kwa chama hicho kwani serikali kushughulika na kero zote ambazo ni kikwazo kwa wananchi.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema alishafuatilia jambo hilo kwa NFRA ili kujua sababu ya usitishwaji huo na kupewa majibu kuwa limesitishwa kutokana na wakulima wengi kupeleka mahindi yao hivyo wanahitaji kufanya utaratibu kwanza wa kuwalipa wananchi hao ndipo waendelee na zoezi la ununuzi kwa wengine.

# UDSM yapewa ekari 1,000 kujenga chuo, hospitali ya kisasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO Kikuu cha Dar es salaam (UDSM), kimekabidhiwa eneo lenye ukubwa wa ekari 1,000 mkoani Mbeya kwa ajili ya kujenga Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi pamoja na hospitali ya kisasa ya kufundishia wanafunzi kwa vitendo.

Eneo hilo lililopo kwenye mashamba ya Tanganyika Pakers katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi limetolewa na serikali ya Mkoa wa Mbeya kufuatia ombi la Mkuu wa Chuo hicho Dk. Jakaya Kikwete ambaye aliomba ekari 500.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo juzi alipozungumza na wazee wadau wa maendeleo wa mkoa huo (WAMAMBE) kwenye kikao cha kujadili mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya mkoa huo.

Alisema awali eneo la kugawa lilikuwa halipo kutokana na kuwepo kwa mvutano wa matumizi ya eneo la Tanganyika Pakers lakini baada ya serikali kuruhusu liendelee kutumika ndipo wakaamua kuligawa.

Alisema Serikali ya Mkoa imekabidhiwa ekari 4,500 kwa ajili ya kuwapatia wawekezaji na hivyo UDSM ni moja kati ya uwekezaji mkubwa ambao umepewa kipaombele.

Mwenyekiti wa WAMAMBE, Polisya Mwaiseje ambaye aliwahi kuwa mbunge wa Mbeya Mjini kupitia Chama cha NCCR Mageuzi aliishukuru serikali ya mkoa huo kwa uamuzi wa kugawa eneo hilo ili mradi huo uanze kutekelezwa.

Alimuomba Homera kumshawishi Rais Samia Suluhu Hassan kwenda kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa chuo hicho ili kuongeza hamasa kwwenye utekelezaji.

Alishauri serikali kulipima eneo hilo na kukipatia chuo hicho ramani ili wapatiwe hati miliki na waendelee na matumizi kwa maelezo kuwa mradi huo ni miongoni mwa miradi ambavyo itaupa heshima mkoa wa Mbeya.

Akizungumza na wazee hao kwa njia ya simu, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Wiliam Anangisye alisema kwa sasa wanaendelea na mchakato wa kujenga chuo hicho baada ya kukabidhiwa eneo hilo.

Hivyo, aliwashukuru wazee wa mkoa huo kwa kupigania kuhakikisha eneo hilo linapatikana na kwamba mradi huo utawanufaisha pia wananchi wa Mkoa wa Mbeya.

# ZMBF kutoa matibabu, uchunguzi wa magonjwa bure

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Maisha Bora Foundation (ZMBF) imeandaa kambi ya matibabu bure kwa wananchi wa visiwani hapa, ambapo watafanya uchunguzi wa maradhi mbalimbali yakiwemo yasioambukiza.

Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Hassan Khamis Hafidh aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa ZMBF, Mama Mariam Mwinyi, anatarajia kuzindua kambi hiyo ambayo itaambatana na matembezi ya hiari ya kilomita tano, yataanzia Manispaa ya Magharib A Unguja hadi viwanja vya Dole.

Hafidh alisema ZMBF kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Afya Check imeona kuna kuweka kambi hiyo ambayo itadumu kwa muda wa siku tatu kuanzia Septemba 30 mwaka huu ili wananchi kupata huduma wanazozihitaji za matibabu ya afya bure.

Alisema katika kambi hiyo wanatarajia kuwafikia zaidi ya wananchi 2,000 kupata matibabu ya afya ikiwemo uchunguzi wa maradhi yasioambukiza kama shinikizo la damu, kisukari, maradhi ya moyo kwa sababu maradhi hayo yanaongoza kwa vifo.

Aidha, alisema kuwa katika kambi hiyo pia kutatolewa huduma ya mama na mtoto kwa kupata vipimo mbalimbali ikiwemo uchunguzi wa maradhi

ya ngozi, macho, kinywa na meno, saratani ya shingo ya kizazi na upimaji wa damu.

Pia, aliwataka wananchi kushiriki kwa wingi katika matembezi na kufika katika kambi hiyo ili kuchunguza afya zao na wale watakaogundulika kuwa na maradhi kupatiwa matibabu mapema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo, Fatma Fungo, alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeingia makubaliano ya kimkakati katika kuimarisha afya ya msingi kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisema lengo kuu la kambi hiyo ni kwenda sambamba na mkakati wa ZMBF wa miaka mitatu ambao una malengo makuu matatu ambayo ni kuimarisha eneo la kiuchumi kwa wakulima wa mwani, kuimarisha afya za kinamama, watoto na vijana kuptia afya ya uzazi, lishe na afya ya mama na mtoto na kumaliza tatizo la udhalilishaji nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A', Suzan Peter Kunambi, alipongeza taasisi hiyo kwa kuamua kuzindua kampeni hiyo muhimu katika wilaya hiyo na mchango anaoutoa katika wilaya hiyo.

"Mama Mariam amekuwa akiunga mkono wilaya yetu ikiwemo kampeni ya chanjo ya UVIKO 19, hii inaonesha kwamba anaunga mkono juhudi za serikali inayoongozwa na Rais Dk. Mwinyi katika kutoa afya kwa wananchi," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Afya Check, Dk. Isaac Kimaro alisema wameamua kuja kushirikiana na ZMBF kupitia kampeni yao na zoezi la upimaji afya bure ambapo dhamira ya mashirikiano hayo ni kuhakikisha kwamba wakazi wa Zanzibar wanapata fursa ya kupatiwa huduma za afya.



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk.Hussein Ali Mwinyi akijumuika na waumini wa Dini ya Kiislamu kuadhimisha Maulid ya Mfungo sita 1445 Hijria sawa na 2023 Miladia, sherehe tukufu ya kuzaliwa na kumuenzi Mtume Muhammad S.A.W katika uwanja wa Maisara, Mkoa wa Mjini Magharibi juzi. **PICHA: IKULU**

# Wazee 25,000 kupewa vitambulisho maalum vya afya, usafiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZEE 25,000 wanatarajiwa kupewa vitambulisho maalum ambavyo vitawarahisishia kupata huduma mbalimbali muhimu kwa haraka ikiwemo afya, usafiri na pensheni jamii ambayo inatolewa na serikali kila mwezi.

Vitambulisho hivyo vitatolewa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi Oktoba moja mwaka huu katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani ambapo yatafanyika huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma alisema serikali itaendelea kuhakikisha wazee hao wanapata huduma za afya bure katika hospitali zote za serikali Unguja na Pemba.

Pembe alisema wizara yake inafuatilia wazee wote ambao hawana vyeti vya kuzaliwa na tayari wameshaingia makubaliano na wakala wa matukio ya kijamii ili wazee hao wanapatiwe vyeti vya kuzaliwa na kupata fursa zinazotolewa na serikali.

"Wizara inaendelea kuratibu pensheni jamii kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kusimamia wazee wasio na vyeti vya kuzaliwa ili kutengenezewa," alisema.

Waziri Pembe alisema hadi Septemba mwaka huu wizara yake inasimamia wazee zaidi ya 29,000 ambao wanapatiwa pensheni jamii kwa Unguja na Pemba.

Akizungumzia siku hiyo alisema Zanzibar inaungana na nchi zingine duniani kuadhimisha siku hiyo kwa shughuli mbalimbali kwa lengo la kuwakutanisha wazee na kuthamini wapi walipo na nini kifanyike ili kuleta ustawi mzuri kwao.

Aidha, alisema katika maadhimisho hayo kutakuwa na maonyesho ya wazee ambapo wataonesha bidhaa na kazi mbalimbali wanazozifanya.

# CHADEMA kufanya kongamano la wazee Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kinatarajia kufanya kongamano mashuhuri la wazee ambalo litawakutanisha wazee wa chama hicho kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambalo litafanyika visiwani Zanzibar.

Kongamano hilo linatarajiwa kufanyika Oktoba moja mwaka huu na litaongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe na litajumuisha viongozi mashuhuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wazee walioshiriki kuikomboa nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa la chama hicho, Idrissa Mzee Said, alisema kongamano hilo litazungumzia masuala ya wazee kwa sababu wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo afya na uchumi.

"Kongamano kama hili tumekuwa tukilifanya kitaifa kila mwaka na huzunguka kila kona ya Tanzania na kwa mara hii tunalifanya visiwani Zanzibar, tunatumia jukwaa hili kuieleza serikali kuchukua wajibu wake katika kutuhudumia sisi wazee"alisema.

Alisema kongamano hilo pia litahudhuriwa na watu mashuhuri bila ya kujali itikadi za vyama vya siasa bali kujali umri, hekima na busara ambapo wataungana pamoja kuzungumzia changamoto za wazee ili serikali kuzifanyia kazi.

Mwenyekiti wa Kanda ya Unguja na Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Said Mzee alisema katika shamrashara za kongamano hilo kutakuwa na matembezi ya hiyari ambayo yataanza katika Bandari ya Malindi hadi ofisi za chama hicho zilizopo Rahaleo Mjini Zanzibar.

Alisema katika kongamano hilo kutakuwa na hotuba za viongozi mbalimbali wakiwemo wagombea wawili wa urais kutoka Chama Cha Mapinduzi na msaidizi wa kwanza wa Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume.

"Tutawapa fursa ya kuzungumza na kutoa uzoefu wao namna gani Mapinduzi ya Zanzibar yalivyokuwa na namna gari Rais wa kwanza wa Zanzibar aliweza kuwajengea makazi wazee wa Zanzibar ambapo hadi sasa wazee wanaishi katika nyumba hizo zilizopo Amani na Sebleni Mjini Unguja"alisema.

Akizungumzia matembezi hayo alisema tayari wamevishirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama na kuviomba kuwa wawe mstari wa mbele katika kuongoza matembezi hayo.

# MATUKIO YA MAULID YA KUZALIWA MTUME MUHAMAD (S.A.W) KATIKA PICHA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Baraza la Maulid Kitaifa kwenye Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Qasida ya Mwaka wa Kiislamu 1445 na Mshauri Mkuu wa Jumuiya ya Milade Nabii Association Zanzibar, Sheikh Sherali Champsi, katika maadhimisho ya Maulid ya Kuzaliwa kwa Mtume Muhamad (S.A.W) viwanja vya Maisara Suleiman Wilaya ya Mjini Unguja jijini Zanzibar juzi usiku. **PICHA: IKULU**




Wanafunzi wa Jumuiya ya Maulidi ya Homu kutoka Mtaa wa Mtendeni, Wilaya ya Mjini Unguja, wakisoma Maulid ya Homu katika maadhimisho ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) katika viwanja vya Maisara Suleiman. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya waumini wa dini ya kiislamu wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipozungumza katika Baraza la Maulid jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**



Wanafunzi wa Madrassatul Sufaiya kutoka Mwanakwerekwe, Wilaya ya Mjini Unguja wakijumuika katika Maadhimisho ya Maulid ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) katika viwanja vya Maisara Suleiman juzi usiku. **PICHA: IKULU**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiongozana na Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Alhaj Mustafa Rajabu Shaban baada ya kuwasili katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete kwa ajili ya Baraza la Maulid kitaifa jana. **PICHA: OWM**

# Rais Kiir afanya ziara Russia

**MOSCOW, Russia**

RAIS wa Sudan Kusini Salva Kiir yuko kwenye ziara nchini Russia kwa ajili ya kukutana na Rais Vladimir Putin.

Ziara hiyo inakuja wakati ambapo Russia na mataifa yenye nguvu ya Magharibi yanajaribu kutafuta uungwaji mkono kwa nchi za Afrika katika vita vinavyoendelea Ukraine.

Rais Kiir aliwasili katika mji mkuu wa Moscow na kupokelewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje Andrey Rudenko Yurevich, kulingana na taarifa kutoka kitengo cha habari cha rais.

Ofisi ya Kiir ilisema mkutano na rais mwenzake wa Russia ulifanyika jana na ulijikita katika matarajio ya maendeleo ya uhusiano baina ya nchi hizo mbili katika maeneo mbalimbali.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa ziara hiyo inalenga kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kuchunguza maeneo mengine ya ushirikiano katika biashara, fursa za uwekezaji na usalama.

Viongozi hao wawili pia walijadili kuondolewa kwa vikwazo vya silaha na vikwazo vilivyowekwa kwa watu binafsi nchini Sudan Kusini.

Mwezi Mei, Russia ilijizuia katika kura ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ya kurejesha vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Sudan Kusini, ambavyo ni pamoja na marufuku ya kusafiri na vikwazo vya silaha.

**BBC**



Kiongozi wa utawala wa kijeshi nchini Burkina Faso Ibrahim Traore akiwapungia wananchi waliojitokeza barabarani. **PICHA: REUTERS**

# Taiwan yazindua nyambizi vita

**TAIPEI, Taiwan**

TAIWAN imezindua manowari yake ya kwanza iliyotengenezwa nchini humo katika mkakati wa kujiimarisha katika ulinzi dhidi ya shambulio linalowezekana kufanywa na China.

Rais Tsai Ing-wen aliongoza hafla ya uzinduzi huo katika mji wa bandari wa Kaohsiung juzi.

Maofisa wa Marekani walionya kuwa China inaweza kuwa na uwezo wa kijeshi kufanya uvamizi ndani ya miaka michache ijayo.

Taiwan ni kisiwa kinachojitawala ambacho China inakichukulia kama jimbo lililoasi na imeapa kukirudisha siku moja.

Waangalizi wengi wanaamini kuwa China haitashambulia kisiwa hicho mara moja, huku nchi hiyo ikisema inatafuta kuungana tena kwa amani na Taiwan.

Hata hivyo, imeonya dhidi ya Taiwan kutangaza rasmi uhuru wake na kutafuta msaada wowote wa kigeni.

Imeendelea kuweka shinikizo kwenye kisiwa hicho kwa kufanya mazoezi ya kijeshi katika Mlango wa bahari wa Taiwan, yakiwemo yaliyofanywa mwezi huu.

Manowari hiyo yenye thamani ya dola bilioni 1.54 inayotumia umeme wa dizeli itafanyiwa majaribio kadhaa na itawasilishwa kwa jeshi la wanamaji kufikia mwisho wa 2024.

**BBC**

# Mapinduzi Burkina Faso yakwama

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

UTAWALA wa kijeshi nchini Burkina Faso, umesema umezuia jaribio la mapinduzi lilotakiwa kufanyika Jumanne ya wiki hii, limezuiwa na watu kadhaa wamekamatwa wakihusishwa na tukio hilo.

Jaribio hilo limetokea ndani ya mwaka mmoja tangu jeshi hilo lilipoingia mamlakani.

Taarifa ya utawala wa jeshi iliyosomwa kupitia kituo cha televisheni cha taifa, ilisema idara za usalama na ujasusi za Burkina Faso zimefanikiwa kuzuia jaribio hilo la mapinduzi lililopangwa kufanyika Septemba 26.

Kulingana na taarifa hiyo, maofisa kadhaa wa jeshi na watu wengine wanaodaiwa kuhusika na jaribio hilo lililonuia kuvuruga utulivu wamekamatwa na wengine bado wanasakwa.

Kiongozi wa kijeshi nchini humo, Ibrahim Traore aliingia madarakani Septemba 30, 2022, baada ya mapinduzi ya pili yaliyofanyika katika kipindi cha miezi minane.

Mapinduzi hayo, kwa sehemu yalichochewa na kutoridhishwa na hatua zilizochukuliwa katika kukomesha uasi wa wanamgambo wa jihadi nchini humo.

Jumanne usiku, maelfu ya watu waliingia katika mitaa ya mji mkuu Ouagadougou kufuatia mwito kuwataka wafuasi wa Traore kujitokeza kumtetea huku uvumi wa mapinduzi ukisambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Taarifa ya utawala huo wa kijeshi ulisema unasikitika kwamba maofisa ambao kiapo chao ni kutetea nchi yao wamepotoka na kutaka kuipindua serikali.

Ilisema hatua hiyo ni kulenga kuzuia maandamano ya watu wa Burkinabe ya kutafuta uhuru na ukombozi kamili kutoka kwa makundi ya kigaidi yanayojaribu kuwafanya kuwa watumwa.

Taarifa zilisema hao walikuwa wakichunguza makazi ya Traore na maofisa wake mwezi huu, mwendesha mashtaka wa utawala huo alisema wanajeshi watatu walikamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kupanga njama dhidi ya utawala huo.

Wachunguzi walidokezwa kwamba wanajeshi wa sasa na wa zamani waliofanyia idara ya ujasusi walikuwa wakiyachunguza makazi na maeneo mengine yanayotumiwa na watu muhimu katika utawala wa kijeshi, ikiwa ni pamoja na Traore mwenyewe.

**DW**

# Armenia yapokea wakimbizi 50,000

**YEREVAN, Armenia**

SERIKALI ya Armenia imesema kuwa imewapokea wakimbizi zaidi ya 50,000 kutoka jimbo la Nagorno-Karabakh ambalo kwa sasa linakaliwa na vikosi vya Azerbaijan.

Hata hivyo, Azerbaijan kwa upande wake iliarifu kumkamata aliyekuwa kiongozi mkuu wa serikali ya jamii ya Waarmenia.

Katika taarifa yake Azerbaijan iliarifu kuwa kiongozi huyo wa zamani anayefahamika kwa jina la Ruben Vardanyan, mwenye umri wa miaka 55 amekamatwa siku ya Jumatano wakati akijaribu kuvuka mpaka kuelekea nchi jirani ya Armenia.

Mke wa Vardanyan, Veronika Zonabend, alithibitisha taarifa ya kukamatwa kwa mume wake ambaye sasa amerejeshwa mjini Baku.

Taarifa ya kukamatwa kwa Vardanyan, ambaye alikuwa mfanyabiashara bilionea nchini Russia na aliyeongoza serikali isiyotambulika rasmi kuanzia mwezi Novemba mwaka 2022 hadi Februari, 2023.

Tangu kuanza kwa operesheni kubwa ya kijeshi ya Azerbaijan, Armenia imetangaza siku ya Jumatano kuwa tayari imewapokea wakimbizi wapatao 50,243 wa Nagorno-Karabakh, ikiwa ni zaidi ya theluthi moja ya wakazi wa jamii hiyo wanaotaka kujitenga.

Siku ya Jumapili, Azerbaijan ilifungua barabara pekee inayotoka eneo hilo kuelekea Armenia, ikiwa ni siku nne baada ya waasi kukubali kuweka chini silaha zao baada ya makubaliano ya kusitisha mapigano.

**DW**

# BOTSWANA KUIJENGA TWIGA STARS KUELEKEA WAFCON

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime amesema atatumia michuano ya Olimpiki kama sehemu ya maandalizi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON 2024) ambapo watakutana dhidi ya Togo.

Twiga Stars itakutana na Botswana katika mechi ya hatua ya pili ya kusaka nafasi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayochezwa baadaye Desemba, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema malengo ya Tanzania ni kupambana kwa ajili ya kupata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za WAFCON 2024 na ni lazima kikosi chake kipate michezo ya kuwajenga.

Shime alisema anajua mechi dhidi ya Togo itakuwa na ushindani kwa sababu kila timu inahitaji kupata tiketi ya kushiriki WAFCON, hivyo wataingia uwanjani wakifahamu kila upande unahitaji kutimiza malengo yake.

"Ni kweli mechi dhidi ya Ivory Coast ilikuwa ngumu sana kwetu, lakini nafurahi vijana wamefanya kile nilichowaambia na kumwondoa Ivory Coast, sasa tunajiandaa na mechi yetu dhidi ya Botswana.

Hii mechi itatusaidia kujiandaa kwa ajili ya mechi yetu ya hatua ya pili dhidi ya Togo na tukifanikiwa kushinda hapo tayari tunaenda kucheza fainali ya WAFCON," Shime alisema.

Kocha huyo aliongeza anafurahi kuona viwango vya wachezaji wake vinaendelea kuimarika na uzoefu wa wachezaji wanaocheza nje ya Tanzania unasaidia kuwapa matokeo mazuri.

Tanzania ilifanikiwa kusonga mbele katika hatua ya pili ya michuano ya WAFCON 2024 baada ya kuifunga Ivory Coast penalti 4-2 kufuatia matokeo ya jumla kuwa mabao 2-2 wakati Togo yenyewe imewaondoa Djibouti kwa kupata ushindi mnono wa mabao 12-1.

Twiga Stars imecheza fainali za WAFCON wakati huo zikiitwa AWC mara moja, ikiwa ni mwaka 2010, fainali hizo zikichezwa Afrika Kusini na ilikuwa chini ya Boniface Mkwasa 'Master'.



Wachezaji vijana wanaolelewa katika Kituo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wakicheza mpira kwenye Uwanja wa Karume jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zimamoto yaitangazia vita JKU

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kikosi chake kuwa na wachezaji majeruhi, Kocha Mkuu wa Maafande wa Zimamoto SC, Mohamed Hilali, amesema wamejipanga vyema kuhakikisha anapata alama tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya JKU utakaochezwa leo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Zimamoto ipo kwenye nafasi ya nne ikiwa na pointi tano baada ya kucheza michezo mitatu.

Akizungumza na Nipashe jana, Hilali alisema anajua anaenda kukutana na timu ngumu hivyo anahitaji kikosi chake kiwe na nguvu za kuwakabili wapinzani wao.

Hilali alisema licha ya majeruhi wengi nyota atakaowapanga watajituma ili wapate matokeo chanya na kuondoka na alama tatu kama ambayo wanatarajia.

"Kikosi changu kiko imara na tayari tumefanya maandalizi yote kuelekea mchezo huu, tumefanya mazoezi yenye hamasa na kuwapa moyo wachezaji ili wapate matokeo mazuri bila ya kuwa na hofu ya mchezo," Hilali alisema.

Kocha huyo pia amewataka mashabiki wa Zimamoto kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo kama ilivyokuwa katika michezo iliyopita.

"Malengo yetu makuu katika msimu huu ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, tumejipanga kurejesha heshima ya klabu yetu," aliongeza Hilali.

## Vijana Queens sasa yafikiria taji la NBL

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kutwaa ubingwa wa kikapu Mkoa wa Dar es Salaam, benchi la ufundi la Vijana Queens limesema sasa linaelekeza nguvu yake katika Ligi ya Taifa (NBL) inayotarajiwa kufanyika kuanzia Oktoba 6, mwaka huu jijini Dodoma.

Kocha Mkuu wa Vijana Queens, Kabola Shomari, alisema ushindani walioupata katika mchezo wa fainali umewaimarisha na watauendeleza katika Ligi ya Taifa.

"Baada ya kupata ubingwa kwa kushinda mechi zote tatu, sasa hivi ninajenga morali ya wachezaji wangu ili wazidi kujiamini na kupambana kutwaa pia ubingwa wa Ligi ya Taifa, tunajua ligi itakuwa na upinzani mkubwa," alisema Shomari.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa kikapu Dar es Salaam (BD), Shendu Mwagala, amesema ligi ya msimu huu imekuwa na msisimko mkubwa tofauti na mwaka jana kutokana na ongezeko la timu za wanawake zilizoshiriki.

Mwagala alizitaka timu zote ambazo hazikufikia malengo zijipange vizuri katika ligi hiyo hapo mwakani.

## Maulid kinara mabao Ligi ya Championship

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mbeya Kwanza ikiwa kileleni katika Ligi ya Championship baada ya kufikisha pointi saba, mchezaji Maulid Khalid wa Mbeya City anaongoza kwa ufungaji mabao.

Khalid amefunga mabao manne mpaka sasa akifuatiwa na Kika Salum wa Pan African ya Dar es Salaam ambaye ana magoli matatu.

Wachezaji 10 wa ligi hiyo kila mmoja amefunga mabao mawili ambao ni Chunga Said na Jacob Benedicto wote kutoka Mbeya Kwanza, Jamal Soud (Pamba), Salim Aiyee (Mbuni FC), Edgar William (KenGold), Kassim Shaibu (Green Warriors), Andrew Raymond (FGA Talents), Makoye Frednand (Mbeya City) na Abdulkarim Segeta anayeichezea Copco.

Ken Gold ya Mbeya inafuatia katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na saba wakati Mbuni FC ikikamata nafasi ya tatu.

Ligi hiyo itaendelea leo kwa Biashara United kutaikaribisha Pamba FC huku Pan African itawaalika TMA kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALONSO KUMRITHI ANCELOTTI
KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi na Xabi Alonso wa Bayer Leverkusen wanawania kuchukua nafasi ya Carlo Ancelotti iwapo ataondoka Real Madrid mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. **(Cadena Ser)**

### SANCHO, HAG HAKUKALIKI
KUNA hisia ndani ya Manchester United kuhusu uhusiano kati ya Kocha, Erik ten Hag na winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 hauwezi kusuluhishwa. **(Mail)**

### OSIMHEN AGOMBEWA ULAYA
KLABU za Saudi Arabia zitaongoza mbio za kumsaka, Victor Osimhen mbele ya Real Madrid na Chelsea iwapo mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24 atashinikiza kuondoka Napoli ifikapo Januari mwakani. **(Mail)**

### UNITED: MEJBRI HAONDOKI
KLABU YA Sevilla imekuwa ikimfuatilia kiungo, Hannibal Mejbri (20), lakini Manchester United inapanga kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mchezaji huyo wa kimataifa wa Tunisia hivi karibuni ili kumbakisha Old Trafford. **(Fabrizio Romano)**

### HAG KUPEWA MKATABA
KLABU ya Manchester United pia inapanga kufanya mazungumzo na Kocha, Erik ten Hag kuhusu mkataba mpya **(90Min)**

### CHELSEA YASAKA MLINZI
CHELSEA iko sokoni kutafuta beki mpya wa kushoto, huku mchezaji wa kimataifa wa Italia na Inter Milan, Federico Dimarco (25) na beki wa AC Milan na Ufaransa, Theo Hernandez (25) wakiwa kwenye orodha yao. **(Calciomercato)**

### WILDER ATAJWA SHEFFIELD
KLABU ya Sheffield United imezungumza na kocha wa zamani Chris Wilder kuhusu uwezekano wa kuchukua nafasi ya Paul Heckingbottom kwa kipindi cha pili cha kuinoa klabu hiyo. **(Football Insider)**

### DIER ANUKIA ROMA
KLABU ya AS Roma inafikiria kumnunua mlinzi wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 29, Eric Dier, katika dirisha dogo ya Januari. **(Calciomercato)**

### EVERTON HALI TETE
HATIMA ya kifedha ya Everton inaweza kuwa shakani ikiwa uchukuaji wa kampuni ya uwekezaji yenye makao yake makuu Marekani ya 777 Partners hautapitishwa. **(Guardian)**

### NEWCASTLE, CASTE WAMALIZANA
KLABU ya Newcastle United ilimaliza mkataba wao wa jezi na mtengenezaji Caste mapema kutokana na wasiwasi kuhusu ubora wa bidhaa zao. **(Mail)**




# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YAJITOSA KUMWANIA OSIMHEN

●●●Lengo ni kutaka kuimarisha safu yake ya ushambuliaji baada ya...

**LONDON, England**

CHELSEA inafuatilia hali ya Victor Osimhen katika klabu ya Napoli baada ya wakala wa mshambuliaji huyo kuwatishia mabingwa hao wa Italia atawashitaki, kwa mujibu wa 90min.

The Blues hao kwa muda mrefu wamekuwa wakimfuatilia mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, ambaye aliiongoza Napoli kutwaa taji lao la kwanza la Serie A katika kipindi cha miaka 33 msimu uliopita.

90min iliripoti Februari, mwaka huu Osimhen ndiye alikuwa mshambuliaji wa kwanza kuwaniwa na Chelsea kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto.

Lakini huku mshambuliaji huyo akionekana kukaribia makubaliano ya mkataba mpya huko Napoli, walibadilisha vipaumbele mahali pengine - Chelsea ilimaliza kusajili wachezaji 12 kabla ya msimu wa 2023/24 badala yake na kumwona Osimhen kama shabaha zaidi ya kufikiwa msimu wa joto mwakani.

Hali sasa inatishia kubadilika, kwani wakala wa Osimhen, Roberto Calenda, amethibitisha wanafikiria kuchukua hatua za kisheria dhidi ya Napoli baada ya klabu hiyo kutuma video inayomdharirisha mshambuliaji huyo kwenye TikTok.

Video hiyo imeondolewa, lakini Osimhen amekasirishwa na namna klabu hiyo ilivyomchukulia.

Calenda alisema : "Kilichotokea katika akaunti rasmi ya Napoli kwenye ukurasa wa TikTok hakikubaliki. Video ya kumdhihaki Victor iliwekwa wazi kwanza na baadaye ikafutwa.

"Jambo kubwa ambalo husababisha madhara makubwa kwa mchezaji. Tunahifadhi haki ya kuchukua hatua za kisheria na mpango wowote muhimu wa kumlinda Victor."

Mapema Jumatano, 90min iliripoti mazungumzo kati ya Osimhen na Napoli juu ya mkataba mpya yalisitishwa.

Mkataba wa Osimhen kwa sasa unaendelea hadi 2025, wakati mkataba wowote mpya huko Napoli ulitarajiwa kuja na kifungu cha kutolewa kwa pauni milioni 150.

Hitaji la Chelsea la kutaka mshambuliaji mpya nyota limekuwa kubwa zaidi kufuatia kuanza kwa msimu mpya vibaya.

The Blues wameshinda mchezo mmoja tu kati ya sita za mwanzo za Ligi Kuu England, wakifunga mabao matano pekee.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,157,2

MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
SEVILLA FC
1 | 1.41
X | 4.96
2 | 7.06

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANTONY KUKUTANA NA POLISI ENGLAND



**MANCHESTER, England**

WINGA wa Manchester United, Antony amerejea England kutoka Brazil na anatarajiwa kukutana na polisi kwa ajili ya tuhuma nyingi za unyanyasaji wa wanawake zinazomkabili.

Antony hajaichezea United tangu walipochapwa mabao 3-1 na Arsenal kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa mapema mwezi huu.

Aliondolewa kwenye kikosi cha Brazil kwa ajili ya mechi zao za kimataifa za Septemba kufuatia madai ya kwanza ya kutoka kwa aliyekuwa mpenzi wake Gabriela Cavallin.

Madai zaidi ya shambulio tangu wakati huo yametolewa na wanawake wengine wawili, Rayssa de Freitas na Ingrid Lana, matukio hayo yakidaiwa kutokea England na Brazil.

90min ilithibitisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 sasa amerejea England, lakini anasalia kwa likizo ya kutokuwapo na kikosi cha United.

Alisafiri Jumanne na anakusudia kushirikiana na Polisi wa Greater Manchester (GMP) kuhusu kuhojiwa.

Tayari ameshirikiana na polisi wa Brazil, ikiwa ni pamoja na mahojiano ya hiari Juni.

Hakujakuwa na mtu aliyekamatwa na hakuna mashtaka yaliyotolewa dhidi ya Antony, ambaye hapo awali alisema kuhusu madai hayo: "Nataka kusisitiza sina hatia kwa mambo ambayo nimekuwa nikishutumiwa."

# Hatima ya Thiago yasubiriwa

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL inafikiria kuamua kuhusu hatima ya kiungo wake, Thiago Alcantara, kwa mujibu wa 90min.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp amekuwa akimpigia debe hadharani Thiago, ambaye aliwasili Anfield kwa shangwe nyingi alipojiunga akitokea Bayern Munich mwaka 2020.

Hata hivyo, muda wa Thiago ndani ya Liverpool umezidi kuandamwa na majeraha na msimu uliopita alianza kwenye mechi 14 pekee za ligi.

Thiago bado hajashirikishwa msimu huu akijaribu kupata nafuu kutokana na jeraha la nyonga alilolipata Aprili, mwaka huu.

90min ianaelewa Thiago aliweka wazi kwa Liverpool hataki kuondoka na alitaka kujiimarisha tena katika safu mpya ya kiungo.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 unaisha msimu ujao wa joto na mazungumzo yamefanyika kuhusu mustakabali wake.

Klopp ni mmoja wa wale wanaotaka kuona Thiago akiongezwa muda, lakini 90min inaelewa kuwa kuna wengine Anfield ambao hawaamini Mhispania huyo ayapata mkataba mpya.



## HABARI MICHEZO


# 90,273/-


# SINGIDA FOUNTAIN GATE YAWAZA MAKUNDI CAF

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Singida Fountain Gate FC, ukisema hautacheza 'kinyonge' huko Misri, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Thambo Senong amesema kikosi chake kina matumaini makubwa ya kutinga hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, imeelezwa.

Singida Fountain Gate itashuka dimbani ugenini Jumapili ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji Future FC katika mechi ya marudiano ya michuano hiyo ya kimataifa.

Thenong aliliambia gazeti hili amewataka wachezaji kusahau matokeo ya mechi ya kwanza na kuingia uwanjani wakiwa na akili mpya ili kufikia malengo yao ya kufuzu hatua ya makundi.

Kocha huyo alisema licha ya kuwa na faida ya bao 1-0 walilopata nyumbani lakini amewasisitiza wachezaji wake kuingia kuongeza umakini katika mchezo huo kwa sababu wenyeji pia watapambana kusaka matokeo mazuri.

Alisema mbali na kuwaona walipocheza nao mechi ya kwanza bado anaendelea kuwafuatilia kwa kutizama mchezo wao wa Ligi Kuu ya Misri, ambao Future ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya El Dakhleg.

"Tumefika salama Misri na tunaendelea na maandalizi dhidi ya Future FC, tumeongea na wachezaji wetu na kuwaeleza tuna kazi kubwa ya kupata matokeo chanya kwenye mechi ya marudiano. Tunaanza upya kusaka matokeo, safu ya ushambuliaji iko imara na kufanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza mechi zilizopita," alisema kocha huyo.



Viongozi wa serikali na vyama vya michezo wa Tanzania, Kenya na Uganda wakiwa katika picha ya pamoja Cairo, Misri wakati wakisubiri kutangazwa kwa mwenyeji wa fainali za AFCON 2027. **PICHA: TFF**

# Simba kuimaliza Dynamos kibabe

INATOKA UK. 24

sababu kila kitu kiko sawa na waamini mechi hiyo itaamuliwa uwanjani.

"Msiwe na wasiwasi wanachama na mashabiki wa Simba, tutacheza mechi hiyo kwenye Uwanja wa Azam Complex na tutaingia makundi, tunakabidhi uwanja wa watu, tunausubiri Uwanja wa Benjamin Mkapa ufunguliwe Oktoba 20, kwa hiyo wasiwe na mashaka hata kidogo," alisema Ahmed.

Aliongeza amewataka mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kwa ajili ya kushangilia kwa sababu timu yao itasonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa.

"Yale ya Jwaneng Galaxy hayawezi kujitokeza tena kwenye maisha ya Simba, katu haitokuja kutokea tena, tunafahamu tulikosea wapi, halitokuja kutokea, tunafahamu kwenye soka kuna matokeo katili lakini kila kitu huwa na sababu yake, sisi kufungwa mechi ile kulikuwa na sababu, tunazijua na tumeshazidhibiti.

Narudia tena hazitojirudia, usitegemee Simba atatolewa na Power Dynamos eti kwa sababu alishawahi kutolewa na wale Wabotswana, ujinga wakati wa kwenda huu ni wakati wa kurudi, sisi tunajua la kumfanya Mzambia," alitamba Ahmed.

Kuhusu wanaosema Simba haichezi soka safi, ofisa huyo alieleza kikubwa timu inashinda na ndio jambo muhimu katika kila mechi.

"Niwaambie tu tutashinda mechi ya Jumapili na tutaingia hatua ya makundi, tutakwenda hadi kufikia malengo yetu ya nusu fainali tukiwa hivyo hivyo hatuna furaha, sisi tunachotaka ni kupata matokeo mazuri na mafanikio siyo kufanya maonyesho, sisi tumeshakuwa timu kubwa, hatufurahishi mtu, tunashinda." aliongeza Ahmed.

## Yanga : Tutatinga makundi

INATOKA UK. 24

towaruhusu Al Merrikh kupata nafasi ya kupata matokeo ambayo yatatufanya tushinfwe kusonga mbele. Malengo yetu ni kutinga hatua ya makundi ya michuano hii," Gamondi aliongeza.

Msimu uliopita Yanga ilishindwa kutinga hatua ya makundi katika mashindano haya ingawa ilifanikiwa kucheza fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/09/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Liverpool FC | 2.80 | 3.90 | 2.15 |
| 02. 30/09/23 | 20:00 | Boavista Porto vs FC Famalicao | 2.17 | 3.30 | 3.15 |
| 03. 30/09/23 | 22:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.21 | 3.15 | 3.25 |
| 04. 30/09/23 | 22:00 | AS Monaco vs Olympique Marseille | 2.20 | 3.65 | 2.85 |
| 05. 01/10/23 | 13:30 | Fatih Karagumruk Istanbul vs Kasimpasa Istanbul | 2.28 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 01/10/23 | 14:30 | FC Nuremberg vs FC Magdeburg | 2.37 | 3.55 | 2.65 |
| 07. 01/10/23 | 14:30 | SV 07 Elversberg vs Greuther Furth | 2.50 | 3.60 | 2.48 |
| 08. 01/10/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Kaiserslautern | 2.65 | 3.45 | 2.42 |
| 09. 01/10/23 | 16:00 | Nottingham Forest vs Brentford FC | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 10. 01/10/23 | 16:00 | Udinese Calcio vs Genoa CFC | 2.08 | 3.20 | 3.45 |
| 11. 01/10/23 | 17:15 | Deportivo Alaves vs CA Osasuna | 2.55 | 3.00 | 2.80 |
| 12. 01/10/23 | 17:30 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.24 | 3.25 | 2.70 |
| 13. 01/10/23 | 18:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.33 | 3.35 | 2.55 |
| 14. 01/10/23 | 18:00 | Hobro IK vs Kolding IF | 2.65 | 3.25 | 2.31 |
| 15. 01/10/23 | 19:00 | Konyaspor vs Besiktas Istanbul | 2.80 | 3.30 | 2.19 |
| 16. 01/10/23 | 19:00 | Viborg FF vs AGF Aarhus | 2.60 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 01/10/23 | 19:00 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.46 | 3.30 | 2.70 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 29/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 1219 | Nantong Zhiyun vs Shanghai SIPG | 5.26 | 4.05 | 1.49 |
| 14:35 | 3903 | Shenzhen vs Changchun Yatai | 9.11 | 5.67 | 1.21 |
| 14:35 | 4158 | Tianjin Teda vs Chengdu Qianbao | 3.39 | 3.28 | 1.96 |
| 16:00 | 1406 | Biashara United vs Pamba SC | 2.70 | 3.25 | 2.30 |
| 18:00 | 1144 | AL Tai vs Al Nasr Riyadh | 10.48 | 6.29 | 1.23 |
| 18:00 | 2361 | VPS Vaasa vs Inter Turku | 1.78 | 3.53 | 3.79 |
| 18:00 | 3761 | AL Hazm vs Al Taawon | 5.23 | 4.08 | 1.58 |
| 18:00 | 4486 | AL Wakrah vs Al Rayyan SC | 2.68 | 3.44 | 2.24 |
| 18:00 | 4576 | Al-Shamal vs Umm-Salal SC | 3.19 | 3.44 | 1.98 |
| 18:00 | 5225 | AC Oulu vs FC KTP | 1.92 | 3.58 | 3.23 |
| 18:30 | 4210 | MSK Zilina vs MFK Skalica | 1.59 | 3.77 | 4.63 |
| 19:00 | 1952 | Rostov vs Ural Yekaterinburg | 2.21 | 3.19 | 3.09 |
| 19:00 | 2908 | Coastal Union vs Kitayosce FC | 1.83 | 3.36 | 4.07 |
| 19:00 | 4542 | Stal Mielec vs Korona Kielce | 2.38 | 3.24 | 2.63 |
| 19:30 | 4442 | Paderborn vs Schalke 04 | 2.16 | 3.76 | 2.86 |
| 19:30 | 5419 | Hamburger SV vs Fortuna Dusseldorf | 1.89 | 3.90 | 3.40 |
| 20:00 | 1447 | Samsunspor vs Gaziantep BB | 1.99 | 3.46 | 3.41 |
| 20:30 | 2044 | FC Wil vs FC Aarau | 2.02 | 3.44 | 3.08 |
| 20:30 | 2482 | Moroka Swallows FC vs Amazulu | 2.25 | 2.85 | 3.10 |
| 21:00 | 1129 | FC Otelul Galati vs Dinamo Bucuresti | 2.33 | 2.98 | 3.08 |
| 21:00 | 1926 | FC Eindhoven vs Dordrecht | 1.76 | 3.69 | 3.89 |
| 21:00 | 3636 | Groningen vs Den Bosch | 1.26 | 5.33 | 8.81 |
| 21:00 | 4033 | MSK Deinze vs RS Waasland Beveren | 2.51 | 3.49 | 2.44 |
| 21:00 | 4333 | Maastricht vs ADO Den Haag | 3.07 | 3.63 | 2.03 |
| 21:00 | 4378 | Telstar vs Jong Ajax | 2.20 | 3.58 | 2.76 |
| 21:00 | 4381 | Jong AZ Alkmaar vs Willem II Tilburg | 3.12 | 3.53 | 2.04 |
| 21:00 | 4530 | De Graafschap vs Roda Kerkrade | 2.16 | 3.47 | 2.91 |
| 21:00 | 5148 | FC Oss vs Emmen | 3.74 | 3.58 | 1.82 |
| 21:00 | 5894 | Al Hilal Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 1.31 | 5.45 | 8.17 |
| 21:00 | 5953 | Cambuur vs Jong PSV | 1.31 | 5.14 | 7.41 |
| 21:15 | 1871 | Neuchatel Xamax vs FC Sion | 3.08 | 3.38 | 2.04 |
| 21:30 | 3496 | Hoffenheim vs Borussia Dortmund | 2.90 | 3.90 | 2.23 |
| 21:30 | 5614 | GKS Piast Gliwice vs Widzew Lodz | 1.55 | 3.63 | 5.24 |
| 21:30 | 5737 | SKN St Polten vs Liebherr Gak | 2.14 | 3.41 | 2.95 |
| 21:45 | 2520 | Dundalk FC vs Drogheda Utd | 1.62 | 3.74 | 4.45 |
| 21:45 | 3056 | Hamilton vs Annan Athletic | 1.42 | 4.20 | 5.80 |
| 21:45 | 3326 | Bohemians FC vs Sligo Rovers | 1.80 | 3.48 | 3.73 |
| 21:45 | 3606 | Galway United vs Athlone Town | 1.26 | 5.25 | 7.87 |
| 21:45 | 4412 | Shamrock Rovers vs Shelbourne | 1.67 | 3.38 | 4.63 |
| 21:45 | 4721 | Bray Wanderers vs Cobh Ramblers | 2.58 | 3.39 | 2.34 |
| 21:45 | 4770 | Waterford Utd vs Wexford Youths | 1.34 | 4.64 | 6.66 |
| 21:45 | 4891 | Cork City vs St Patricks | 3.33 | 3.38 | 1.95 |
| 21:45 | 5251 | Kortrijk vs Cercle Brugge | 4.39 | 3.99 | 1.65 |
| 21:45 | 5994 | Derry City vs UCD Dublin | 1.10 | 7.01 | 17.95 |
| 22:00 | 1896 | Strasbourg vs Lens | 3.24 | 3.39 | 2.24 |
| 22:00 | 2617 | Barcelona vs Sevilla FC | 1.41 | 4.96 | 7.06 |
| 22:00 | 2865 | Leganes vs Racing Santander | 2.16 | 3.07 | 3.32 |
| 22:00 | 4072 | Sheffield Wed vs Sunderland | 2.96 | 3.31 | 2.22 |
| 22:00 | 5718 | Finn Harps vs Kerry FC | 1.50 | 4.06 | 5.07 |
| 22:15 | 3940 | Benfica vs Porto | 2.02 | 3.44 | 3.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Septemba 29, 2023
Nipashe





Chelsea yajitosa kumwania Osimhen UKURASA 21



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (aliyesimama), akizungumza na wachezaji wa Singida Fountain Gate (pichani kulia), ambao keshokutwa watawavaa wenyeji Future FC ya Misri katika mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: SINGIDA FG**

# YANGA: TUTATINGA HIVI MAKUNDI CAF

## ●●●Gamondi afunguka tiketi ya kucheza makundi imebebwa na...

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha timu yake inasonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema amehamishia nguvu katika safu yake ya ulinzi kwa sababu anaamini ndiyo imebeba tiketi yao ya kutinga hatua ya makundi.

Yanga inatarajia kuikaribisha Al Merrikh kutoka Sudan katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watashuka dimbani kesho wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata ugenini katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki iliyopita.

Safu ya ulinzi ya Yanga inaongozwa na nahodha, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Bacca, Attohoula Yao na Dickson Job.

Katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika juzi na jana kwenye Uwanja wa Avic Town, ulioko Kigamboni, Gamondi alikuwa makini zaidi kuwapa maelekezo mabeki wake kwa lengo la kuwaimarisha na kujiandaa kupunguza makosa yanayozalishwa na mipira ya kutenga.



Akizungumza na gazeti hili jana, Gamondi alisema ingawa mabeki wake hawajaruhusu bao katika mechi za ushindani lakini anahitaji walinzi hao kuongeza umakini zaidi kuelekea mchezo huo wa kimataifa.

Gamondi alisema anatarajia mechi hiyo ya marudiano itakuwa na ushindani kwa sababu wapinzani wao Al Merrikh wataingia tofauti ili kulipa kisasi.

Kocha huyo alisema bado mabeki wake wanafanya makosa katika mipira ya kutenga na anataka kuona tatizo hilo linamalizika ili kuwadhibiti wapinzani wao Al Merrikh.

Alisema si vizuri kuona walinzi wanafanya makosa katika eneo la hatari, ni bora makosa madogo yafanyike katika maeneo mengine kwa sababu ni hatari na yanaweza kuwapa faina wapinzani.

"Tunatakiwa kuongeza umakini katika eneo la hatari, mipira ya kutenga sio mizuri, wachezaji wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa sababu katika mpira lolote linaweza kutokea, tusiruhusu kufunga.

Tumepata matokeo mazuri katika mechi ya kwanza lakini hatulazimiki kuridhika, ninaimani Al Merrikh wataingia kivingine kwa sababu ya wao kutaka kupata matokeo," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisisitiza walifanikiwa kupata mabao 2-0 ugenini, anatarajia hata wapinzani wao wana uwezo wa kushinda endapo hawatakuwa makini kwa kuruhusu wacheze na kufanya mashambulizi.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi hii ya marudiano, ninataka kuona tunawafunga na pia ku-

UKURASA. 23

# Simba SC kuimaliza Dynamos kibabe

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimesalia siku mbili kuelekea mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos kutoka Zambia, mabosi wa Simba wamewaondoa wasiwasi mashabiki na wanachama wao kwa kusema 'mipango yote muhimu' imekamilika.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Ndola, Zambia, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2.

Hata hivyo baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo wamekuwa na wasiwasi na hawataki kukumbuka yaliyotokea katika mechi zilizopita dhidi ya UD Songo ya Msumbiji na Jwaneng Galaxy ya Botswana yanajirudia.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana kuelekea mechi hiyo, klabu yao imekamilisha maandalizi yote yanayohitajika ya ndani na nje ya uwanja.

Ahmed alisema wamejipanga kudhibiti hujuma na wawe na subira kwa

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042